# *Kusikia, Kupokea, Na Kutenda*

Asanteni sana. Mnaweza kuketi. Ndugu Clair Hutchins alisema atanipiga risasi, naye akapita nayo. Ni vizuri sana kuwa hapa usiku wa leo, Ndugu Winston. Nami nadhani Ndugu Mattsson yuko hapa mahali fulani, na . . . [Ndugu Joseph Mattsson-Boze anasema, "Hapa!"—Mh.] Vema, nina furaha kukuona, Ndugu Mattsson, tena, niliuliza habari zako jana jioni. Vizuri sana, hilo linanifanya nijisikie vizuri sana, kuwaona wengi sana, na Ndugu Clair Hutchins, na kuleta salamu kutoka ng'ambo. Ajabu!

2 Jana jioni, ninaamini ya kwamba David du Plessis . . . Simwoni. Nilifikiri ningeangalia kote kwanza na kuona kama ningeweza kuona . . . Huyu *hapa*. Ninaamini alilitendea kusanyiko hili udhalimu wakati tulipokuwa tukienda zetu nyumbani. Tukaingia kwenye gari pamoja, nami nikaangalia chini, nikasema, "Loo, ni karibu saa nne." Nikasema, "Ndugu David," nikasema, "Nadhani niliwaweka watu hao kwa muda mrefu kupita kiasi."

3 Akasema, "Ndugu Branham, nafikiri hao watu wanajisikia karibu kama ninavyojisikia, tumechoshwa na kusikia mahubiri duni, ya wahubiri duni, kwa Wakristo duni."

4 Kwa hiyo, hilo huenda likanitia moyo kuhubiri saa mbili zaidi usiku wa leo, kwa hiyo . . . La, kwa kawaida nitawaachilia kabla ya saa saba. Kamwe sikuninii . . . Lakini nilikuwa sininii, tunaanza tu vizuri saa saba. Tungekaa na kumsifu Bwana usiku kucha. Ni vibaya sana kwamba tuliyaacha hayo, sivyo? Hakika ni vibaya, Ndugu Sullivan. Halafu tukaingilia mahubiri ya kiakili ya dakika ishirini, nami nashangaa tu hayo yote yanatoka wapi. Sijui kama kidogo hatujaribu kujifananisha na ulimwengu kupita kiasi. Ninaamini kama hilo halijafaulu sana katika safu zetu, nafikiri yatupasa tuliondokee.

5 Mwajua, ninapenda tu kuketi, na kutafuna, na kula, na kutafuna, na kula ninapokuwa mezani; nami, ninapokuwa kwenye meza ya Bwana, ninapenda kukaa muda mrefu. Mchungaji wetu hivi majuzi usiku, alihubiri yapata dakika arobaini na tano, ninamwona akiangalia juu kwenye saa, nami nafikiri, "Naam, Ndugu Neville, unaingia ndani yake, pia." Mnaona? Dakika arobaini na tano, huo si muda wa kutosha kuanza. Tunapaswa kuwa na, mimi . . . Yeye anakuwa, anakuwa tu wa kupendeza, nilikuwa tu nikichochewa kufikia

mahali ambapo nilikuwa nikijisikia vizuri sana, mwajua, ndipo akaukatiza. Ni aibu jinsi gani!

6 Lakini sasa, kila siku kuna ibada huku nje, nami ninajua nyote mna wakati mzuri sana. Ni watu wangapi hapa ambao hawatoki Ohio? Hebu tuone mikono yenu, watu wasiotoka Ohio. Ajabu! Hilo ni sawa. Nadhani zaidi ya nusu ya kusanyiko hili wanatoka nje ya jimbo la Ohio. Hakika tuna furaha kuwa nanyi hapa. Ombeni kwamba Mungu atazidisha baraka Zake kwenu. Naomba mwende nyumbani, mrudi kwenye mikoa yenu ya nyumbani mkishangilia, mkiwa na furaha, mkimsifu Bwana.

7 Sasa, nataka, usiku wa leo, kusoma Maandiko yanayopatikana katika Warumi mlango wa 8, nasi tutaanza kusoma hapa yapata kifungu cha 11, cha mlango wa 9, hasa. Hebu tuanzie kwenye yapata kifungu cha 10:

> *Wala si hivyo tu; lakini Rebeka naye. . .kuchukua mimba kwa mume mmoja, naye ni Isaka, baba yetu;*
>
> *(Kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia yake yeye aitaye;)*
>
> *Aliambiwa hivi, Mkubwa atamtumikia mdogo.*
>
> *Kama ilivyoandikwa, Nimempenda Yakobo, na Esau nimemchukia.*

8 Ningetaka kuchukua somo kutoka hapo, juu ya yapata maneno matatu: *Kusikia, Kupokea, Na Kutenda.*

9 Kabla hatujalikaribia, hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapozungumza kwa muda kidogo na Mwandishi wake.

10 Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, tunakushukuru usiku wa leo kwa ajili ya yote ambayo Wewe umetufanyia, kwa ajili ya wema Wako na wingi wa rehema Zako ambazo zimemwagwa juu yetu kwa neema Yako. Si kwamba tumefanya lolote kuzistahili, bali kwa sababu Wewe umekuwa mwema kwetu, wala hujaangalia udhalimu wetu, bali umetupa vipimo visivyo na kikomo vya neema Yako. Tunakushukuru kwa ajili yake.

11 Na kama tunavyosikia usiku wa leo, ukija uwanjani, ushuhuda wa madaktari, ukinena juu ya wale ambao walikuwa wafe majuma machache yaliyopita na sasa mahali hapo pameponywa, madaktari na wauguzi wakituma ujumbe, "Mwambie atuombee," hilo linaifanya mioyo yetu kujisikia vizuri sana, Bwana. Nasi tunawaombea hao madaktari na hao wauguzi, ambao wako tayari na wanatambua kwamba mkono wa Mungu uliingia na kutenda kazi juu ya mtu huyu wakati walipokuwa wamemhesabu kuwa amekufa, ama alikuwa anaenda kufa, sasa yu hai na ni mzima. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili!

12 Halafu jana jioni kuona safu hii kubwa ya watu wakienda taratibu kwenye safu kuingia chumbani wapate kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Wako, kuwaona wenye dhambi wamesimama hapa madhabahuni wakilia, wazee kwa vijana, kwa jumla inaifurahisha mioyo isivyoweza kuelezeka kwa maneno. Hakika, Wewe ungali ni Mungu mkuu wa Mbinguni.

13 Tungeomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe ungebariki kusomwa kwa Neno, na naomba utupe muktadha wa somo hili, usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu aje na kufasiri Neno hili mioyoni mwetu. Jalia sasa tuvute mapazia yaliyotuzunguka kutoka kwa ulimwengu wa nje, na kuishi tu huku mioyo yetu imeelekezwa Kwako. Jalia mioyo yetu ifunguliwe, na jalia msukumo wa Roho uwe mkubwa sana katika jengo hili usiku wa leo, mpaka atakapojiingiza Mwenyewe katika kila ufa na kona ya mioyo yetu, akiijaza kila sehemu iliyo safi na tayari kwa kujazwa.

14 Naomba umponye kila mgonjwa aliye hapa, uokoe kila nafsi iliyopotea, na ujaze kila moyo wenye njaa na Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

15 Wavuvie watumishi Wako, wahudumu, ndugu zetu wapendwa na wa thamani, wachungaji wa kundi, ambao umewaita na kuwatenga, maisha yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya huduma. Tunawaombea, Bwana, kwa kuwa hao ndio watu watakaowabeba hawa, wenye nyumba ya wageni watakaowachukua watu hawa wagonjwa, wa nafsi na mwili, na kuendelea kuwamiminia Mafuta na divai mpaka wapate afya. Inasemwa katika ule mfano kwamba aliwapa peni mbili, ambazo zilikuwa kwa ajili ya wokovu na uponyaji pia, na kusema, "Kama kuna kitu kingine cha zaidi, nitalipa nitakapopitia hapa tena."

16 Na kama tukipungukiwa na chochote leo, Bwana, ambalo tunajua tumepungukiwa, tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatupa hicho, usiku wa leo, tulichopungukiwa nacho. Tusaidie sisi wahudumu, Bwana, ili tuweze kuwatumikia watu Wako kwa dhamiri safi na moyo safi. Tujalie, Baba. Tunaomba haya kwa unyenyekevu sana, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

17 Ulimwengu siku hizi umeshikwa na nguvu mbili kuu, nguvu mbili kuu za kidini ambazo hivi karibuni zinakuja kwenye kilele au shindano la kuamua. Zimewakilishwa vizuri katika somo letu la Maandiko usiku wa leo, la wana wawili wa Isaka, Esau na Yakobo. Na wakati . . . Wanawakilisha nguvu hizi zote mbili, na zote zinatoka kwa baba mmoja na mama mmoja.

18 Yule mtakatifu aliyechaguliwa tangu zamani na Mungu, Isaka, na Mungu alimwambia baba yake miaka ishirini na mitano kabla hajazaliwa, angempata mtoto huyu, kwa mama aliyetengwa na kuwekwa wakfu, Rebeka, bikira. Nao hawa wana wawili walikuwa katika tumbo moja. Walikuja

ulimwenguni wakizozana na kupigana, wakiwa vitani mmoja na mwenzake, wamekuwa wakipigana tangu wakati huo, na wangali watapigana mpaka wakati wa mwisho. Nao ulimwengu umeshikwa kabisa usiku wa leo katika nguvu hizi.

19 Sasa, matamshi yanayonibidi kutamka, na baadhi ya Maandiko niliyoandika hapa, na kadhalika, ninataka kila mtu ajue ya kwamba wakati mwingine ninaporejea kwenye hali ya kanisa, ama dhehebu, ama chochote kile, mara nyingi ndugu zangu hunichukua vibaya ninaposema hivyo. Sizungumzii watu waliojazwa na Roho wanaosimama kama wachungaji na kulilisha kundi la Mungu, ambao wamechaguliwa na Roho Mtakatifu kufanya hivyo, ninazungumza juu ya waaminio wa kimwili, wanaojaribu kupachukua mahali pa watu hawa.

20 Nasi tunaona ya kwamba Esau kweli alimwakilisha mwaminio wa kimwili. Yeye alikuwa mtu wa duniani, na alikuwa wa duniani, naye alikuwa na mwelekeo wa kidini sana, alikuwa na dini yake kama tu ulimwengu ulivyo nayo siku hizi. Karibu watu wote unaozungumza nao, wana dini ya namna fulani, kama wanahudhuria kanisa lao ama la, lakini wao, labda mara moja kwa mwaka, ama wanawake wanapenda kwenda kwenye Pasaka kuonyesha kofia zao mpya, nao wanaume wanapenda kwenda mara moja moja wakati wanapokuwa na jambo fulani linaloendelea ambalo litawatumbuiza. Nao walikuwa, wangali ni mtoto mchanga, wananyunyiziwa na jina kuandikwa kwenye kitabu cha kanisa, nao ni mali ya kanisa.

21 Kamwe nisingeweza kuliendea hilo. Sisi. . .Mwanadamu si mali ya kanisa, wala mwanadamu si mali ya serikali, mwanadamu ni mali ya Mungu, wana na binti za Mungu, sisi ni mali Yake kwa sababu tumenunuliwa kwa Gharama. Na ni Gharama ya thamani jinsi gani, Mwana wa Mungu!

22 Lakini Esau aliwakilisha vizuri kundi hilo la kuwa watu wa kidini, na, “Mimi ni mzuri tu kama huyo mwingine.” Na, “Dini yangu ni nzuri kama yako, nami nimeridhika kabisa.”

23 Lakini Yakobo, ndugu yake pacha, kwa kuchaguliwa, ambaye alikuwa kwa kuchaguliwa tangu zamani kwa kujua tangu zamani, alikuja ulimwenguni naye alikuwa mtu wa kiroho kuwakilisha watu wa kiroho. Naye alikuwa, alikuwa na upambanuzi wa kiroho wa yaliyokuwa mema na yaliyokuwa mabaya. Na kama mtaelewa, ya kwamba Kanisa lote la Mungu aliye hai limejengwa juu ya ufunuo wa Yesu Kristo. Habili alimtoleaje Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini kama hakufunuliwa ni nini dhabihu iliyohitajika, ni dhabihu gani iliyohitajika, hasa?

24 Wanafunzi walipoulizwa, “Ninyi mwasema, Mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

25 Petro, bila kusitasita, alilipuka kama mtu anayenena kwa lugha, kasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

26 Yesu akasema, “Heri wewe, Simoni, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, hukujifunza hili kupitia mpango wowote wa elimu ya kiakili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu,” si juu ya Petro, si juu yake Mwenyewe, bali juu ya ufunuo wa kiroho ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani, “juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

27 Ilionyesha yangelipinga, bali kamwe hayatalishinda. Kwa hiyo Kanisa litaninii, Kanisa la kiroho litasonga mbele moja kwa moja kuingia katika Umilele, kwa hakika tu kama vile kulivyo na Mungu aliyelikusudia liwepo.

28 Kwa hiyo ni utoshelevu ulioje inayotupa kujua basi, kwamba mnapozaliwa na Roho wa Mungu, ninyi ni wana na binti za Mungu.

29 Sasa huyu, Yakobo, ilimaanisha mengi sana kwake, bali ile haki ya mzaliwa wa kwanza haikuwa na maana yoyote kwa Esau, kusema kweli, yeye aliidharau. Nami nasema hili kwa uchaji wote: watoto wake wangali wanaidharau. Hiyo ni kweli. Anaidharau. “Kwa nini mimi . . .? Yanibidi kufanya hivyo kwa sababu gani? Kwa nini nimpokee Roho Mtakatifu? Mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe, dini yangu ni nzuri kama yako. Kwa nini nipitie hayo yote hapo? Mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe, ninaenda kanisani, jina langu liko kwenye kitabu. Mimi ninaninii tu . . . Mimi ni *fulani-wa-fulani*.”

30 Hivyo—hivyo ndivyo ulivyo, lakini wewe ni nini machoni pa Mungu? Huna budi kuzaliwa mara ya pili, mwenye akili ya kiroho.

31 Kwa hiyo haikumaanisha chochote kwa Esau, aliidharau. Naye mwaminio wa kimwili siku hizi angali anaidharau Haki hiyo ya Mzaliwa wa kwanza. Nayo Haki ya mzaliwa wa kwanza ni Roho Mtakatifu, tu—tunajua hilo, naye mwaminio wa kimwili humdharau Huyo. Loo, akasema, “Siku hizo zimepita. Hakuna kitu kama kumpokea Roho Mtakatifu tena, hiyo ilikuwa katika, huko nyuma katika wakati wa mitume.”

32 Nilimsikia mtu mashuhuri akisema wakati mmoja katika kanisa zuri, yeye alisema, “Pentekoste ilikuwa tu kazi ya jukwaa kwa jengo,” kisha akasema, “basi baada ya jengo kujengwa, mbona,” kasema, “hawahitaji hilo jukwaa tena.”

33 Kwa hiyo, mwishoni mwa ibada, nikazunguka kuja kupeana mikono na mtu huyu mashuhuri, nikasema, “Ninataka kukupongeza kwa ujumbe wako asubuhi ya leo, Daktari.” Nikasema, “Nitakubaliana nawe ya kwamba Pentekoste ilikuwa ni kazi ya jukwaa, na mradi tu tunajenga juu yake, bado

hatuna budi kuwa na jukwaa." Hiyo ni kweli. Jukwaa ndicho kitu cha mwisho cha kubomolewa. Mpaka utakapoweka ninii—mwisho wa mnara-pia juu yake, kileleni, ingali inakubidi kuwa na hilo jukwaa. Nina furaha usiku wa leo, kuendelea kufanya kazi katika hili jengo, nikisimama jukwaani basi, sivyo?

34 Sasa, tunaona ya kwamba haki hii ya mzaliwa wa kwanza ilimaanisha kila kitu kwa Yakobo. Sasa, yeye hakujali kitu kingine, ila haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Hakujali ilimgharimu nini, kama ilikuwa ni sehemu ya mlo wa dengu, alifurahia kumrudishia Esau. Ndivyo ilivyo na mwanamume yeyote ama mwanamke aliyekusudiwa Uzima wa Milele, ambaye Mungu amemwitia Uzima wa Milele, yuko tayari kuuza chochote, chochote cha ulimwengu apate hiyo Haki ya mzaliwa wa kwanza.

35 Unaweza kuwaita chochote utakacho, unaweza kuwaambia wamerukwa na akili, wameingia wazimu, kundi la watakatifu wanaojibingirisha, sijali mnawaitaje, wanaitafuta hiyo Haki ya mzaliwa wa kwanza, na hiyo inamaanisha zaidi ya kitu kingine chochote. Wanaifuata hiyo Haki ya mzaliwa wa kwanza, haidhuru itawalazimu kuipataje, wako tayari kuipata.

36 Mtu wa kimwili anataka Mungu ashushe Haki ya mzaliwa wa kwanza kwenye kiwango chao. Lakini kwangu mimi, na ninaamini Wakristo wote waliozaliwa kikweli, tunakutana Nayo kwenye kiwango cha Mungu. Sijali yanipasayo kufanya, ama yanipasayo kusema, inipasavyo kutenda, jambo pekee, ninaitaka. Hiyo inamaanisha zaidi ya umaarufu wangu, hiyo inamaanisha zaidi ya kazi yangu, inamaanisha zaidi ya mama yangu, inamaanisha zaidi ya mke wangu, zaidi ya watoto wangu, zaidi ya kila rafiki niliye naye, hebu nipate hiyo Haki ya mzaliwa wa kwanza, sijali yanipasayo kulipa.

37 Ninataka kukutana na Mungu kwa masharti Yake. Chochote anachohitaji, kama ni kuanguka mavumbini, kama ni kunena kwa lugha, kama ni kukimbia-kimbia jengoni na kutenda kama mwendawazimu, ama kusimama kwa kichwa changu, sijali ni nini, bora tu nimpate, hilo ndilo jambo muhimu. Hao ni watu wenye nia ya kiroho, wanataka ile Haki ya mzaliwa wa kwanza, wanaitaka, haidhuru.

38 Na mara tu wanapoipata, inatenda vile vile ilivyotenda katika familia hiyo. Hatimaye, itafikia mahali ambapo utengano utakatokea. Itambidi mtu kupata, kama akiipata Haki hii ya mzaliwa wa kwanza, itambidi kujitenga na ulimwengu, kama tu vile ilivyomlazimu Yakobo kujitenga.

39 Jamani, wakati mwingine inamaanisha kutembea peke yako. Lakini kama wewe kweli ni mwaminifu, na kweli umepokea Haki ya mzaliwa wa kwanza, hujali kutembea peke yako. Ikiwa majirani hawatakualika tena kwenye chakula cha jioni, kama hakuna mtu atakayekuwa na uhusiano wowote nawe, inaleta

tofauti gani kwako? Mradi una Haki ya mzaliwa wa kwanza, hayo ndiyo mafanikio makuu ya maisha yako.

40 Maadamu nimezaliwa na Roho Mtakatifu, inaleta tofauti gani? Maadamu niko njiani kwenda Mbinguni, inaleta tofauti gani yale watu wanayosema, mradi tu tunatembea katika Roho? Na wote waliozaliwa na Roho wa Mungu, wanaongozwa na Roho wa Mungu. Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu, daima wakitembea katika nuru nzuri ya utakatifu, usafi.

41 Lakini Esau, hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa, alikuwa wa kimwili kama ulimwengu, kwa hiyo haikuleta tofauti yoyote kwake. Alifikiri alikuwa wa kidini, na baba yake na mama yake walikuwa wa kidini, na hilo lilitosha kabisa kwake.

42 Kwa hiyo tunaona ya kwamba katika kila uamsho uliowahi kuzaliwa ulimwenguni, unazaa mapacha, hiyo ni kweli, kila uamsho una mapacha. Wana kundi mle ndani ambalo ni waaminio wa kimwili, na kundi la waaminio wa kiroho, kila uamsho huwazaa hao, Esau na Yakobo.

43 Basi wanapoendelea, muda si muda mwajua, wa kimwili anaanza kuwazia, "Vema, jamaa hawa wanaanza kuingia wazimu, afadhali nijitenge nao." Wanarudi kwenye sehemu ya kiakili. Wanataka mchungaji atakayewazungumzia mambo ya kupendeza. Hawamtaki huyo mchungaji aliyejazwa na Roho, ambaye atamtii Roho Mtakatifu kutoka jukwaani, anayehubiri tu Neno jinsi tu lilivyo.

44 Kama Yohana alivyosema, "Weka shoka kwenye shina la mti, acha vibanzi vianguke, mahali vitakapo." Makanisa mengi siku hizi watalitoa hilo mimbarani mwao kwa kura. Hiyo ni kweli. Utakuja utengano, hufanya hivyo kila mara. Ilifanya wakati wa Kimethodisti, ilifanya wakati wa Kibaptisti, ilifanya wakati wa Kipentekoste, itafanya katika kila wakati.

45 Wakati mmoja John Wesley, nilikuwa nikisoma makala, juu yake, nayo yalisema kwamba alikuwa akishuka kwenye njia ndogo, naye kwa namna fulani alikuwa akilishutumu kanisa la Kianglikana juu ya dhambi yao, na mambo waliyokuwa nayo, waliyokuwa wakifanya. Nao wakamwita m—mwendawazimu. "Basi wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watapitia mateso," ungedharauliwa na kukataliwa. "Na kama wakimwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi Wake?"

46 Basi kulikuwako na mmoja wa hawa maafisa wa kanisa la Kianglikana, mtu mkubwa mno, akamwona John akija, naye alikuwa ni mtu mdogo, kwa hiyo jamaa huyu mkubwa akamfungia njia moja kwa moja. Bw. Wesley akaja karibu naye, wala asingeweza kumkaribia, akasema, "Samahani, bwana. Waweza kusogea kando, ili niweze kupita?"

Mtu huyu akasema, "Kamwe simpishi mpumbavu."

47 Bw. Wesley kwa heshima akainua kofia yake, akaenda nyuma yake, na kusema, “Sikuzote mimi humpisha.” Kwa hiyo, nafikiri hilo karibu latosha. Yeye sikuzote humpisha.

48 Sasa, tofauti hizi daima zimekuwako tangu Kaini na Habili. Kaini na Habili, wanadamu wa kwanza walioleta uhai duniani, Adamu na Hawa walizaa wawili, mmoja wa aina moja na mwingine wa nyingine. Kulikuwako na Kaini na Habili; kulikuwako na Esau na Yakobo, kulikuwako . . . kote kuendelea, daima imekuwa hivyo, hizo roho mbili zikipigana makanisani, tumekuwa nayo kwa wingi sana.

49 Na daima hufikia mahali ambapo inabidi kuwe na wa—wakati wa utengano. Ibrahimu na Lutu walianza kuutafuta ule Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake alikuwa ni Mungu. Lutu alikuwa mtu wa kimwili, ndipo hatimaye ikafikia mahali ambapo ilibidi Ibrahimu na Lutu watengane kabla kamwe hawajaweza, Ibrahimu hajaweza kuipata ile ahadi. Iliwabidi kutengana, mmoja na mwenzake.

50 Na ndivyo ilivyo usiku wa leo, huna budi kujitenga na mambo ya ulimwengu, huna budi kutembea pamoja na Wakristo. Mimi ni mwaminio hodari katika Wakristo kushirikiana na Wakristo. Naam, bwana. Hamwezi kutembea pamoja msipokubaliana, na mlikubaliana kwanza na Kristo, na kila mtu anayekubaliana ndani ya Kristo, atakubaliana nawe.

51 Basi Ibrahimu na Lutu iliwabidi kutengana kabla Mungu hajambariki Ibrahimu. Naye Lutu, mliona hiyo hali ya kimwili? Hata hivyo kama—kama mshiriki vuguvugu wa kanisa, alijua ya kwamba Ibrahimu alikuwa akiishi huko juu katika hema, lakini mliona, dini yake ilikuwa nyofu sana, hata Lutu hakumwomba yule Malaika, “Jalia nikwee pamoja na Ibrahimu, amu wangu,” lakini alisema, “Kuna mji mdogo hapa chini, mimi . . . niruhusu niende kwenye huo”? Bado hakutaka uhusiano wowote na Ibrahimu.

52 Mnaona, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, hata ufanye nini, wa kimwili hawawezi kushirikiana na wa kiroho, si zaidi ya vile unavyoweza kuchanganya mafuta na maji, hayatachanganyikana.

53 Kwa hiyo, kanisa linahitaji utakaso mzuri. Tunachohitaji siku hizi ni miamsho ya mtindo wa kale, uamsho wa kufagia, nguvu fulani za Bwana. Tunahitaji wanaume na wanawake ambao wako tayari kuuza kila kitu katika ulimwengu huu, kuchoma kila daraja nyuma yao.

54 Tunahitaji kuuteka ulimwengu siku hizi, sisi wahudumu, kama vile Wanorwe wa kale walivyokuwa wakiiteka nchi. Walipoingia kwa meli, walifika ufukoni na kuiwasha moto hiyo meli na kuiteketeza nyuma yao, hawakuwa na njia ya kutorokea. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, kuchoma kila daraja na kila njia ya kutorokea, kuuza kila kitu kwa ajili ya Ufalme

wa Mungu na kuendelea kusonga mbele. Hakuna mahali pa kusimama, hakuna mahali pa kupatana.

55 Mungu hawapendi wanaopatana. Mungu hataki Kanisa Lake lifanane na ulimwengu, hataki litende kama ulimwengu, hataki kuwa na uhusiano wowote na ulimwengu, ila tu kuwahubiria walimwengu Injili na kuwaita hao.

56 Mungu anataka watenganishaji; kanisa linataka wachanganyaji. Wanataka mchungaji ambaye hatakuwa mkali sana kwao, na—na kuwaambia mambo mazuri, na asichimbue ndani sana na kuwachuna tu ngozi. Ndugu, hilo ndilo tunalohitaji.

57 Hapa majuma machache yaliyopita mahali fulani, nilipata ono, na kulikuwa na mtoto wa paka amelala juu ya m—mto nami nilikuwa nikimpapasa namna *hiyo*, naye alikuwa tu akikoroma, nami nikaona juu yake, alikuwa na jina. Nami nilifikiri yeye ndiye maskini jamaa mwenye sura nzuri sana, naye alikuwa tu akikoroma, kana kwamba alikuwa amelala. Ndipo Roho akasema, "Hebu mpapase kinyumenyume mara moja."

58 Nilipompapasa kinyumenyume, kule kukoroma kote na kupiga kelele uliowahi kusikia, hayo macho ya kijani kibichi yakiangaza, alikuwa ni mnyama wa kuchukiza kuliko wote niliyepata kumwona.

59 Loo, maadamu unaweza kuwaacha watu waende vyovyote watakavyo, watakupa katinipu, sawa, lakini inapofikia mahali. . .Hatuhitaji katinipu, tunahitaji nguvu za Roho Mtakatifu zirudi kanisani, na zirudi jengoni, Uhai uliofufuka wa Yesu Kristo unaotusafisha, unaotufanya viumbe vipya. Tunahitaji divai kali, si katinipu, hiyo ni kwa ajili ya watoto wachanga.

60 Mama yetu alikuwa akiwapa watoto, nafikiri, namna fulani ya katinipu, walipoumwa na tumbo. Kanisa lina zaidi ya kuumwa na tumbo, lina upungufu wa damu. Tunachohitaji ni kutiwa damu, nguvu za Roho Mtakatifu kuusafisha ulimwengu wa kanisa kutokana na maisha ya dhambi.

61 Wanawake, wanaume, wanaokiri Ukristo, huko nje kwenye dansi, huko nje kwenye karamu kubwa, za kilimwengu, kucheza kamari, kuvuta sigara, kucheza dansi, wanawake wakikata nywele zao, wakivaa kaptura, suruali ndefu, namna zote za upuuzi kama huo, na halafu wajiite Wakristo? Kuna udhaifu mahali fulani, hauko katika nguvu za Mungu, uko katika mimbara yenu, ama ndani yenu, mojawapo. Sasa, ni hayo tu, ni kweli. Tunahitaji kusafishwa. Wa kimwili, daima ni uadui.

62 Loo, hakika, ni vita vikali, bali ninaamini kama umekusudiwa Uzima wa Milele, "Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu."

63 Sasa, unasema, "Vema, mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe."

64 Lakini, ndugu, utahukumiwa kwa kazi ulizofanya. Kazi zako zinaenda . . . zinathibitisha kile ulicho.

65 Mtu fulani aliniambia wakati fulani uliopita, kasema, "Kama nikihukumiwa kwa imani yangu, nimeokoka; kama nikihukumiwa kwa matendo yangu, nimepotea."

66 Nikasema, "Matendo yako yanathibitisha imani yako." Hiyo ni kweli. Kama unampenda Bwana, uta—utaingia moja kwa moja na kila kitu asemacho Mungu, nawe utadumu moja kwa moja nacho.

67 Nia ya kimwili italiambia Neno la Mungu, loo, mhudumu huyo mwenye elimu, aliyefunzwa vizuri atasema, "Loo, sasa angalieni, enyi watoto, hilo ni ushupavu wa dini, msiliamini hilo, hamna kitu hapo. Msiliamini hilo." Hiyo kweli ni katinipu, sasa, ninawaambia hiyo itawafanya walale usingizi.

68 Lakini mtumishi halisi wa Mungu atairarua hiyo ngozi kutoka kwako. Naam, bwana. Atakutikisa kwa Neno la Mungu, naye atakwambia yaliyo kweli na yaliyo mabaya. Asipofanya hivyo, nisingetoa hela kwa mahubiri yake, hiyo ni kweli kabisa.

69 Mtu yeyote anayeogopa riziki yake, ama *chochote kile*, ambao hawatasimama na kusema kweli ya Neno la Mungu, anachohitaji ni kuingia katika mkutano wa Kipentekoste wakati mwingine na kupata mjazo halisi wa Kipentekoste, ambao utalishughulikia.

70 Vema, ni kama baadhi ya watu hao ambao iliwabidi kuacha kila kitu walichokuwa nacho wapate kutembea na Bwana. Lakini ilikuwa ni kitu gani? Walichaguliwa na Mungu. Hawajali walichopaswa kuacha. Methodisti, Baptisti, Presbiteri, wanatoka kila mahali . . .

71 David du Plessis anaweza kuwaambia mambo hayo vizuri kuliko niwezavyo, anayafahamu vizuri zaidi. Lakini atawaambia katika jumbe zake, ya kwamba ni jambo la kutikisa. Ndugu du Plessis anajulikana sana kila mahali miongoni mwa makundi ya wasomi, naye Mungu katika siku hizi za mwisho anawaita hao watu watoke, Methodisti, Baptisti, Wapresbiteri.

72 Hebu nikwambie, rafiki Mpentekoste, afadhali uwe chonjo, "Kwa maana Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mungu atatenda kazi, atakuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, atakuwa na kitu anachoweza kuweka mikono Yake juu yake, na kusema, "Hao ni Wangu, hilo ni Kanisa Langu, hao ni watu Wangu. Umewatazama watu Wangu?" kama alivyomwambia Ayubu. "Hakuna aliye kama wao duniani, wao ni wakamilifu, hakika. Wananiishia Mimi, hawajali mambo ya ulimwengu, waliyatatua hayo muda mrefu uliopita. Ninaweza kumwambia *huyu*, 'Nenda,' naye ataenda; na *huyu*, 'Njoo,' naye atakuja."

73 Unajua, huwezi kuwa na jambo hili, huwezi kulielewa, mpaka lifunuliwe kwako. Jambo lote limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho, inakubidi kusikia, na halafu utambue, na kisha utende. Limefunuliwa kwa baadhi wala si kwa wengine: Mtu mmoja anaweza kusoma, "Yesu Kristo yeye yule jana, na hata milele."

Nia ya kimwili inasema, "Vema, kwa njia moja ndivyo alivyo."

Nia ya kiroho itasema, "Ndivyo alivyo kwa *kila* njia."

74 Yesu alitoa agizo: "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Nia ya kimwili inasema, "Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Mitume."

Nia ya kiroho itasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. 'Ulimwenguni kote,' nami ni sehemu yake." Naam.

75 Watu Wake ni watu wa kipekee, watu wa kiroho, watu waliotengwa, Kanisa Lake. Neno lenyewe *kanisa*, linamaanisha, "walioitwa watoke," Mungu aliliita Kanisa Lake litoke, maana yake, "walioitwa kutoka ulimwenguni," wasiwe pamoja na ulimwengu tena. Jitenge na mambo ya ulimwengu.

76 Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Haidhuru ni mfuasi mzuri jinsi gani wa kanisa, hilo halina uhusiano wowote nalo. Ingawaje, wanaume wanapaswa kuwa wafuasi wa kanisa, wanawake wanapaswa kuwa wafuasi wa kanisa, watoto, sisi sote, tunapaswa kuwa wafuasi wa kanisa, lakini kwanza lazima tuwe katika Kanisa la mzaliwa wa Kwanza, tuzaliwe katika Kanisa la Mungu.

77 Sasa, tunaona ya kwamba funuo hizi huja, na mtu anazisikia, anazitambua kuwa ni Mungu, kisha anazitekeleza; nia ya kimwili huzisikia, na kusema, "Upumbavu," na kuachana nazo.

78 Sasa, ungeweza kuwazia huko nyuma kabisa katika wakati wa Biblia, wakati Nuhu alipokuwa huko nje shambani mwake siku moja, naye alikuwa ni mkulima, ndipo akasikia Sauti ya Mungu, Sauti ya Mungu ikasema, "Kutakuwa na mvua, itaifunika dunia nzima. Nitaangamiza uovu wote wa ulimwengu huu, hauna budi kufika mwisho."

79 Ungeweza kuwazia Nuhu akipanda juu, na kusema, "Vema, huenda, labda afadhali nijijengee safina, kwa sababu huenda ikanyesha"? La. Neno la Mungu lilifunuliwa kwake. Mbona, kama angalilichukua tu namna hiyo, mwenye kudhihaki wa kwanza aliyekuja, na kusema, "Vema, mwangalie maskini yule mtakatifu anayejibingirisha," angekitupa kitu hicho chote juu, kasema, "Jamani, hebu tuachane nacho."

80 Hivyo ndivyo watu wafanyavyo unaposema, “Nilianza, ibilisi—ibilisi akanifanya nirudi nyuma.”

81 Ibilisi hakulifanya, ulilifanya mwenyewe. Kila mtu amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa na kupimwa, bila shaka wanajaribiwa. Mwaminio halisi amesikia Neno la Mungu, amelitambua kuwa ni Neno la Mungu, atalitekeleza, hivyo tu.

82 Sasa, Nuhu, la hasha. Wenye kudhihaki walikuja na kumdhihaki; akaendelea kuitwanga ile safina. Kwa nini? Alikuwa na hakika kwamba Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu alilosikia. Alilitambua kuwa ni Mungu, naye akalitekeleza. Alikuwa akitenda, nalo likatimia, kwa sababu Mungu alisema hivyo, bila shaka.

83 Tungeweza kumwazia Musa? Ungeweza kuwazia Musa huko nje akisema, “Vema, nitakwambia nini, ninaamini sasa, nitashuka kwenda Misri tena ambako nilishindwa wakati mmoja. Nimekuwa nikisoma sana saikolojia, nami ninaamini kweli ningeweza kumwelezea maskini Farao. Ninaamini ninayo. . . Ningeweza kuchukua digrii nyingine. Ninaamini kama—kama ningalikuwa tu mahali fulani ambapo ningeweza kuipata, ningeweza. . . wangenipa digrii nyingine, labda B.A., ama—ama D.D., ama kitu fulani; hu—huenda wakanipa kitu kingine”?

84 Ungeweza kuwazia Musa akisema hivyo, wakati kwanza kabisa elimu yake ilikuwa imemwingiza katika shida? Lakini shida yake ni kwamba siku hizi, kanisa linaingia katika hali hiyo, nia ya kimwili.

85 Hivi mlijua ya kwamba Musa alikuwa ni mmishenari? Na, mwajua, kwamba makanisa mengi siku hizi, ndiyo kwanza nisikie ya kwamba kabla mmishenari hajatumwa nje, kanisa limtume nje, hana budi kuchunguzwa na daktari wa akili kuona kama ana nguvu za akili za kutosha, kuona kama nguvu zake ziko sawa katika mitazamo ya akili kabla hajaweza kwenda.

86 Ungeweza kuwazia Musa akisema, “Afadhali nishuke niende hapa chini mahali fulani na kujitafutia daktari wa akili sasa, aone kama nina nguvu—nguvu za akili zinazofaa kwenda Misri au la”?

87 Hebu niwaambie, hiyo si huko nje tu katika ulimwengu wa kawaida wa kanisa, hiyo ni katika Pentekoste. Ungeweza kuwazia ikimbidi Musa kusimama mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili aone kama ataweza kushuka kwenda, kuiteka Misri baada ya kuisikia Sauti ya Mungu? La, bwana. Hakuna mtu anayepaswa kufanya hivyo. Madaktari wa magonjwa ya akili sio wanaowaita watu, Mungu huwaita watu; Roho Mtakatifu ndiye anayewatuma watu. Kanisa linapofikia mahali hapo, limerudi nyuma, vibaya sana. Naam, bwana. Lakini watakuwa hivyo, wao ni wasomi.

88 Mungu humwita mtu, anamfanya mmishenari. Biblia ilisema kitu cha kwanza ni mitume, hao ni wamishenari, cha pili ni manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti, na kadhalika. "Mungu aliweka Kanisani," si shirika la madaktari, bali Roho Mtakatifu wa Mungu aliweka Kanisani, wamishenari, na manabii, wachungaji, waalimu, na wainjilisti, Mungu aliwaweka Kanisani. Haikuwabidi kusimama mbele ya mtaalamu yeyote wa magonjwa ya akili, kamwe hawakusimama, kamwe hawatasimama.

89 Mungu humpa mtu ujumbe, anausikia, anautambua kuwa ni Mungu, kisha anautekeleza. Si kazi ya mtu mwingine, ni kazi yake. Mungu alimtuma kazi ya Mungu, yuko kwenye shughuli ya Mfalme. Na kila kitu kinapaswa kumpisha Mfalme. Hiyo ni kweli.

90 Ukienda Uingereza, uanze kushuka mtaani, uwe na ujumbe, "Kwenye shughuli ya mfalme," kila polisi atatoa maelekezo kwa watumia barabara, chochote kile, maana uko kwenye shughuli ya malkia. Hiyo ni kweli. Nchi yoyote iliyo na mfalme, mradi unafanya shughuli yao una haki ya kupita.

91 Nawaambia, tunapaswa kuwa, usiku wa leo, na haki ya kupita. Na hebu niwaambie jambo fulani, ndugu, watake wasitake kulitambua (Hili hapa linakuja.), tuna haki ya kupita. Amina. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu hutoa haki ya kupita, kama tu ukiweka kifua chako mbele, na kuinua kichwa chako, na kusonga mbele. Amina.

92 Ninajisikia usiku wa leo, Ndugu Sullivan, kama Yoshua na Kalebu walivyojisikia, "Tunaweza hata na zaidi kuiteka." Tunaweza hata na zaidi kuwa na uamsho halisi wa Kipentekoste wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu. Mungu alitoa ahadi, "Katika siku za mwisho nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili." Tunaweza hata na zaidi kufanya jambo hilo. Ubora uko papa hapa, papa hapa chini usiku wa leo, kuna karama za kila namna, kila namna za nguvu za Mungu, jambo pekee, kwa namna fulani tumerudishwa nyuma kwake. Lishindanie moja kwa moja. Amina. Mungu hataki waoga.

93 Maskini Yoshua aliunyamazisha huo umati, na kusema, "Simameni kimya kwa dakika moja! Kundi hili la waaminio wakwamia mpakani hapa, tayari wameonja zabibu za Kanaani, halafu wanaogopa hatuwezi kuiteka. Mungu alituahidi huko chini miaka mia nne iliyopita, kwamba tungeweza kuiteka, tunaweza hata na zaidi kuiteka." Hao wakaingia katika ile nchi na kuiteka.

94 Hakuna hata mmoja wa hao walionung'unika aliyepata kuingia katika nchi hiyo, naye Yesu akasema, "Wamekufa." *Kufa*, hiyo ni kusema, "Kutengwa milele." Kasema, "Wao ni . . . "

Akasema, "Baba zetu walikula mana jangwani kwa muda wa miaka arobaini."

95 Akasema, “Na wote wamekufa. Lakini mimi ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni, mtu akila Chakula hiki, ataishi milele.” Amina.

96 Ni Chakula tofauti jinsi gani tulicho nacho siku hizi! Pamoja na Chakula hiki tunachopata, kinapaswa kukupa uti wa mgongo kama gogo la kuchana mbao, na kuweka maarifa mengi pembeni mwa ukuta wa nafsi yako, na kama vile Buddy Robinson alivyosema, “Hebu nipigane na ibilisi mradi tu nina jino, kisha nimwume kwa ufizi mpaka nife.” Simama pale juu, na, na kupigana na kitu hicho mpaka kwenye mtulinga.

97 Unasema, “Lakini, Ndugu Branham, kamwe siwezi kutupa sigara hizi chini.”

98 La, hujagonga—hujagonga. . .hujapata tiba sahihi bado, hujapata tu tiba yake, bado. Hebu mwingize tu Roho Mtakatifu humo ndani, uone jinsi unavyoweza kufanya jambo hilo basi.

Useme, “Kamwe siwezi kujizuia kufanya jambo *hili*.”

99 Loo, hujapata tu—hujapata tu kitu kifaacho bado. Kama vile Daudi katika Agano la Kale, mwajua, alisema, “Kuna asali mwambani.”

100 Mnajua ilikuwa kwamba mikoba yao midogo, walibeba asali kidogo. Ko—kondoo akishikwa na ugonjwa, wangechukua asali hii na kuiweka juu ya mwamba wa chokaa, ili kondoo waurambe huo mwamba. Basi alipoiramba hiyo asali kutoka mwambani, akameza chokaa kwa kuilamba ile asali, nayo ikamtibu huyo kondoo mgonjwa. Sasa, hilo ndilo tunalohitaji.

101 Sasa angalia, ndugu, nina mkoba mzima uliojaa hiyo hapa, nami nitaweka asali hii hapa kwenye Mwamba, Kristo Yesu, si juu ya kitu kingine, bali juu ya Kristo Yesu, nanyi kondoo wagonjwa mtaramba. Nami ninawaambia, wakati mnapoiramba hiyo asali, inua mikono yako na kumsifu, hivyo ndivyo unavyofanya hilo, na humo ndani, mtapata chokaa kiasi.

102 Mtapata baadhi ya nguvu za Mungu za uponyaji, mtasamehewa baadhi ya dhambi, si baadhi, bali zote, nanyi mtampata Roho Mtakatifu. Wakati ukiiramba hiyo asali, jambo fulani litatendeka kwako, itakutenga na mambo ya ulimwengu, nayo itayaita kitu duni, upate kumwishia Kristo, kumfanyia Kristo, bila shaka. Naam, bwana.

103 Musa? Mbona, bila shaka, hakuenda kwenye shule fulani ama kusimama mbele ya mwanasaikolojia fulani aone kama angeweza kushuka kwenda Misri. Alikuwa ameiona Nguzo hiyo ya Moto, imezungushwa kwenye kilele cha kichaka, ndipo alipoona jambo hilo, aliwazia, “Unajua nini?” Ilivutia usikivu wake.

104 Kwa hiyo, akaanza kusikia Sauti ikitoka pale, ikisema, “Nimesikia vilio vya watu Wangu, nami nimelikumbuka agano Langu, nami nimeshuka ili niwakomboe.”

105 Jambo la kwanza alilofanya, alisikia, kisha akatambua ilikuwa ni Mungu, kwa sababu ilikuwa ni Neno. Sasa, tunapoona mambo yakiendelea, yachunguzeni kwa Neno. Kama Mungu akitoa ahadi katika Neno, Mungu atatuma hiyo kuiunga mkono. Amina.

106 Loo, ndugu, loo jinsi ninavyopenda hilo! Hilo lilinigusa, nilipata asali wakati huo. Naam, bwana. Loo, jinsi anavyofanya jambo hilo!

107 Yeye—Yeye alikuwa amemwahidi baba ya Ibrahimu, ama Ibrahimu baba ya Musa, hasa, alisema ya kwamba watu wake wangekaa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne, bali Yeye angewatoa tena. Naye Ibrahimu alijua ya kwamba Mungu angefanya hivyo. Na sasa, huyu hapa Musa, mamia ya miaka baadaye, naye akasikia Sauti hiyo, nayo hiyo Sauti iliyokuwa ikisema naye, ilikuwa ni Maandiko kabisa, kwa hiyo alikuwa anatenda. Amina. Haya basi. Amina.

108 Mungu aliahidi kwenye Siku ya Pentekoste, wakati hao watu walipoanza kupiga mayowe, "Waume na ndugu, tufanye nini?"

109 Petro akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Haleluya!

110 Ninaona kanisa likinena kwa lugha, likipaza sauti, likimsifu Mungu, likitabiri, na kufanya miujiza mikubwa na ishara, ninaangalia chini katika Maandiko, ni ahadi, ndipo nikasikia, nikatambua, nami nikaingia kazini. Amina. Nimekuwa kazini kwa miaka thelathini na mmoja, ndugu. Utukufu! Ninajisikia vizuri, ninajisikia kubarikiwa sana. Amina. Iliniingiza katika matendo.

111 Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu afanyavyo. Husemi, "Itanibidi kufanya nini?" Jisalimishe tu, Yeye atashughulikia yaliyosalia. Niliingia katika matendo, Musa alikuwa katika matendo, inakufanya ufanye vituko wakati mwingine, hakika inakufanya.

112 Ungeweza kuwazia mzee mmoja sasa, mwenye umri wa miaka themanini, masharubu yamening'inia chini namna *hii*, na labda nywele zinaning'inia begani mwake, huku mke wake ameketi akimtagaa maskini nyumbu mzee, akiwa na mtoto chini ya mkono wake, mtoto wake mchanga, naye huyu hapa, maskini fimbo iliyopinda mkononi mwake, akichechemaa tu?

Baadhi ya wachungaji waseme, "Kwani unaenda wapi, Musa?"

"Nashuka kwenda Misri kuiteka." Ni dhihaka jinsi gani kwa watu wa kimwili!

Wanasema, “Maskini mzee Musa, nadhani kachomwa na jua kupita kiasi, hivyo tu.”

113 La, huenda jua halikuwa na joto sana, j-u-a, M-w-a-n-a alimkaribia, hivyo ndivyo ilivyokuwa, ile Nguzo ya Moto ilikuwa kwenye kichaka kilichowaka moto. Mnakumbuka Yesu alisema Yeye alikuwa ndiye Mtu huyo, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Hiyo ni kweli.

114 Sasa, mkiangalia, Mungu hutoa ahadi, halafu Roho Wake ajapo, anaitimiza ahadi hiyo. Sasa, wewe. . .Jambo la kwanza unapolisikia likihubiriwa, basi unatambua ya kwamba hiyo ni kweli ya Mungu, ndipo unaingia kazini. Nia ya kimwili huwazia kwamba umerukwa na akili kabisa.

115 Lakini hilo jambo, hilo lilionekana kama uvamizi wa mtu mmoja akishuka kwenda Misri, kama mtu mmoja akienda kule, kuiteka Urusi. Mbona, hakika, hilo ni jambo lile lile. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba, alifanya hivyo. Kwa nini? Alisikia Sauti ifaayo, akaitambua, na akatii.

116 Nawe unasema, “Siwezi kufanya hivyo.”

117 Naam, unaweza. Kama Mungu akisema nawe, utambue kuwa ni ahadi Yake, ingia kazini, uone yale Mungu afanyayo, tutaiteka.

118 Kiwete anasema, “Siwezi kutembea.”

119 Naam, unaweza, Yesu alisema hivyo. Amina. Hiyo ni kweli. “Yoyote mtakayo, mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, yatakuwa yenu.”

120 Labda mtu aliye na kansa anasema, “Siwezi kuishi.”

121 Naam, unaweza, Mungu alisema hivyo.

122 “Aisee, Musa, ati unashuka kwenda kuiteka Misri? Mbona, haiwezekani!”

“Nitaiteka, kwa vyovyote vile.”

“Utatumia—utatumia silaha ya aina gani?”

“Fimbo hii.” Fimbo ya kale, iliyopinda! Loo, jamani!

“Utatumia silaha ya aina gani?”

123 Mbona, bila shaka. Jambo ni kwamba, Mungu alisema hivyo, hilo lilitosha. Mungu anaposema hivyo, nia ya kiroho inalishika, na hilo tu ndilo wanalohitaji. Haikumlazimu kufanyiwa uchunguzi na daktari wa tiba wala mtaalamu wa magonjwa ya akili kuona kama aliweza, alikuwa na nguvu za akili kufanya hivyo, Mungu alimwambia hivyo, na hilo lilitosha, kwa hiyo akaendelea. Hivyo ndivyo kila mwaminio alivyo, wanaamini tu yale Mungu anayowaambia, kama yako katika Neno, Biblia ilisema hivyo.

124 Kama vile wakati ninyi Wapentekoste mlipoanza kwa mara ya kwanza yapata miaka hamsini iliyopita, kwa nini makanisa

yalisema ninyi ni kundi la wapumbavu, “Mbona lingepoa katika saa ishirini na nne.” Kasema, “Hakutakuwa na chochote kwa hilo.”

125 Ni kitu gani? Huh! Halipoi, linawaka moto. Amina. Kanisa la Kipentekoste linasonga mbele, waongofu wengi mno. Gazeti la *Mgeni wa Jumapili* la Katoliki lilikuwa nayo hapa si muda mrefu uliopita, kwamba walikuwa na waongofu wengi kuliko kanisa lingine lolote lililokuwako ulimwenguni katika muda wa mwaka mmoja. Ni kitu gani? Watu walioshika moto, watu ambao wamekuwa karibu na kichaka kilichowaka moto, watu ambao wamesikia, wametambua, na wanatenda kulingana na Neno Lake.

126 Hawajali wanaitwaje, ni Haki ya mzaliwa wa kwanza. Hawajali yale. . .inawabidi kuhubiri wapi, kama ni pembeni mwa barabara, ama huko nje kwenye kitalu, ama popote ilipo, wataihubiri Injili, kwa sababu wamesikia na kutambua kwamba ni Mungu, nao wakalitekeleza, ndipo Roho Mtakatifu akaja. Mioyo yao inawaka kwa bidii, hawana budi kwenda, vijana au wazee, ama chochote kile, yeye anaingia uwanjani, kwa sababu gani? Mungu alimwita. Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

127 Vipi kama ulimpeleka Eliya kwenye Mlima Karmeli? Wakati, hebu umwazie huko juu na watu hawa wengine wote wakiomba, na kusema, “Loo, Baalimu njoo ufanye mambo fulani.”

128 Akasema, “Nichinjieni maksai na muwalaze pale,” kisha maji yote yakaletwa yakamwagiliwa pale.

129 Huenda waliwazia, “Vema, maskini jamaa huyo mzee. Mnajua, kuna kasoro.”

130 Labda Eliya, kama Mungu hakuwa amesema naye, huenda alisema, “Sasa, ngoja kidogo, afadhali niwe na hakika ya jambo hili, labda Moto huo hautashuka.”

131 Loo, msingeweza kumwazia Eliya akisema hivyo, maana Mungu alikuwa amemwambia hivyo, akatambua ilikuwa ni Sauti ya Mungu. Akasema, “Nileteeni mapipa ya maji. Mwageni hayo mapipa ya maji juu yake. Ninajua Moto utashuka.” Kwa nini? Ilimbidi kuweka mambo katika utaratibu. Alikuwa amesikia, a—akapokea, naye alikuwa akitekeleza yale Mungu aliyosema yafanywe.

132 Kama huamini Mungu atakupa Roho Mtakatifu, lisikie, litambue, upande hapa na uone kama atakupa au hatakupa. Wewe njoo na moyo safi, njoo ukiwa na nia safi, na kujisalimisha kwake, nawe uliamini kwa moyo wako wote, uone kinachotukia. Naam, bwana. Kama si wazo la kiakili la kitu fulani cha kiakili ambacho umekuwa nacho, kama Mungu, chini moyoni mwako anakuita, atakujaza na Roho Mtakatifu hakika kama vile jina langu lilivyo Bill Branham. Hakika atafanya hivyo, utaweka katika matendo yale unayosikia, na kutambua kwamba ni Mungu.

133 Lakini sasa mradi tu unasema, "Vema, huenda isiwe. Hu—huenda ikawa labda mhubiri huyo ananiambia jambo baya. Labda mimi . . . "

134 Mtu fulani aliniandikia hapa si muda mrefu uliopita, na kusema, "Ndugu Branham," kasema, "Hebu nikwambie, sote tunakuamini wewe kuwa ni nabii." Kasema, "Maadamu Roho wa Bwana yuko juu yako, nawe unawapambanua watu na mambo kama hayo, upambanuzi huo, tunajua huyo ni nabii. Lakini," kasema, "mafundisho yako ni mabaya sana. La!"

135 Mbona, ndugu, hata hujui maana ya nabii. Neno la Bwana humjia nani? Nabii. *Nabii* maana yake nini? Kwa jumla halimaanishi m—mtabiri, ama mwonaji wa mambo ya mbele, ama msema yajayo, ama mwenye kubashiri, *nabii* maana yake ni hivi: "kwamba amepewa hiyo kuthibitisha kwamba yeye ni mfasiri wa Neno la Kiungu." Kabisa. Utukufu! Mnawezaje kuwa na msimamo mkali hivi? Inaonyesha ninyi ni wa kimwili, watu wanapofanya hivyo.

136 Wana kanuni ndogo ya imani, ama chochote kile, wanachoshikilia, kwamba wataenda wasome katekismo hii, ama waseme *jambo lingine*, lakini inapofikia kwenye Neno la Mungu, ndugu, hawajui zaidi juu Yake kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Sasa, hiyo ni kweli.

137 Roho Mtakatifu anashuhudia; Mungu hutuma ishara na maajabu. Hiyo ndiyo sababu mnaona mikutano ya uponyaji miongoni mwa Wapentekoste, walimpokea Roho Mtakatifu, kuna *kitu fulani* ndani yao kinachowaambia ya kwamba Mungu ni halisi. Wanakiangalia, wanakiamini.

138 Hiyo ndiyo sababu Wamethodisti na Wabaptisti wanatoka, Mungu amewaita. "Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Haleluya! Najisikia kuendelea na safari. Naam. "Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli. Mungu anabisha, wewe jibu tu.

139 Sasa, Eliya alisema, "Nimefanya haya yote kwa amri Yako. Yale uliyoniamuru kufanya, Bwana, nimeyafanya. Niliisikia Sauti Yako, nikatambua ilikuwa ni Wewe, nami ninatenda. Hakuna Moto ulioshuka bado, lakini huyu hapa fahali, haya hapa maji, haya hapa mawe, hapa kuna kila kitu, kila mtu ananipinga, ninasimama peke yangu, lakini ninafanya kazi." Amina. Whiu!

140 "Mama alisema kama nikienda mkutanoni tena, angenifukuza kutoka nyumbani. Baba alisema angekuja na kunifukuza nitoke mkutanoni na kunikanyaga, lakini Bwana mimi huyu hapa, ninasikia, ninatambua, ninatenda." Jambo ndilo hilo. Amina.

141 "Mume alisema atanifukuza." "Mke alisema nisingeweza kurudi nyumbani tena." Inaleta tofauti gani? Unasikia, unatambua, na unatenda. Amina. Sijali yale majirani wasemayo,

yale mtu mwingine yeyote asemayo, lisikie, litambue, na kuliweka katika matendo. Amina.

142 Eliya akasema, "Nimefanya haya yote kwa amri Yako, Bwana. Kama tu vile ulivyoniambia, nilikusikia, nilitambua ilikuwa ni Wewe, nami ninaliweka katika matendo. Sasa, hilo hapo. Bwana, na ijulikane leo, ya kwamba nimesema kweli na huyu ni Wewe." Na yapata wakati huo Moto ukaanza kushuka.

143 Weka tu mambo tayari. Sikia Neno la Mungu, na ujue ni ahadi ya Mungu.

144 Mungu alimwahidi Eliya angefanya hivyo. Hakuna, hapakuwapo na makuhani wa kutosha nchini humo kumshawishi asifanye hivyo, hakuna wa kutosha—hakuna ufalme wa kutosha katika Ahabu kumdanganyia. Alijua Mungu alikuwa. . . Alikuwa amemsikia Mungu, alitambua ilikuwa ni Mungu, alikuwa akitenda yale hasa Mungu aliyomwambia afanye. Hivyo ndivyo inavyokupasa kuja. Hiyo ni . . .

145 Kama mkutano huu, kama mkutano huu wa Kipentekoste wenu ninyi ndugu msio na mipaka ya kimadhehebu, na ndugu wa kimadhehebu, na yeyote uliye, Wapentekoste, laiti ungalitambua ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, kabla tu ya Kuja kwa Bwana, laiti ungalitambua ya kwamba makanisa yetu yanalundikana, ya kawaida na ya kiroho yanakutana katika mapambano hayo, haina budi kuwa hivyo, hiyo ndiyo sababu Mungu anaita kutoka kwa Methodisti, Baptisti, Katoliki, Wapresbiteri, wowote wale, wanampokea Roho Mtakatifu, kwa sababu ni Mungu akitenda kazi, wanatenda kazi, laiti tungalilipata ono hilo, kungekuwako na uamsho utakaoanza kwenye uwanja huu wa kambi nasi hatungeondoka hapa tena. Hiyo ni kweli. Ungekuwa ni wakati mzuri sana, kama tungeweza kusikia, na kutambua ya kwamba ni ahadi ya Mungu, "Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili."

146 Loo, laiti ungaliweza tu kutambua ni ahadi ya Mungu! "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Haidhuru ulimwengu wa kiakili unasema nini, hu—hushirikiani na hilo. Mlisikia, mlitambua lilikuwa ni Neno la Mungu, kwa sababu liko katika Biblia, basi mnaliweka katika matendo.

147 Ninakumbuka baba yangu mwenyewe alinifukuza nyumbani, nilitia nguo zangu kwenye gunia la karatasi, akasema, "Huwezi kufanya hivyo hapa."

148 Nikasema, "Kuna ulimwengu mzima, mkubwa hapa, wa kutendea hayo," kwa hiyo ni—nikaondoka. Hakika. Nilikuwa na Roho Mtakatifu, kitu fulani kikiwaka moyoni mwangu. Nilikuwa nimesikia, nikaliamini, nikalipokea, nilitambua ilikuwa ni ahadi ya Mungu, "Nami nitaimwaga Roho Yangu . . . Ishara hizi zitafuatana na hao . . . Ahadi hii ni kwa ajili yenu na

kwa watoto wenu . . . " Huyo alikuwa ni mimi. "Yeyote atakaye na aje . . . " Huyo alikuwa ni mimi.

149 Nilivaa miwani mikubwa mno, minene, kichwa changu kilitetemeka wakati wote kwa austigmati, nilikuwa mvulana tu, kitu kama hicho, bali niliamini uponyaji wa Kiungu. Kwa nini? Niliusikia. Nikatambua ilikuwa ni ahadi ya Mungu.

150 Nilienda kwenye kanisa langu mwenyewe la Kibaptisti, na kumwambia Mchungaji, "Una mafuta ya kupaka?"

Akasema, "Unatafuta nini kwenye mafuta ya kupaka?"

Nikasema, "Ninataka kupakwa mafuta."

Kasema, "Ya nini?"

Nikasema, "Mimi ni mgonjwa."

"Una shida gani."

Nikasema, "Siwezi, macho yangu yana shida, sioni vizuri. Nivue miwani hii, ndiposa itabidi waniongoze kila mahali, austigmati."

"Loo," akasema, "Billy . . . "

Nikasema, "Hiyo ni kweli. Huna yoyote, nitakuletea kidogo."

151 Nikashuka, nikanunua mafuta kidogo, nikayaombea, nikaja na kumpa. Akanipaka mafuta namna hiyo, nikasema, "Haleluya!" Mimi hapa nikaenda. Hivyo tu.

152 Daktari alisema kama nikila mdomo mmoja wa chakula kigumu, kingeniua, kasema tumbo langu halikuwa kitu ila kidonda kimoja kikubwa, kilichojaa damu. Ndipo nikaenda nyumbani, naye Baba alikuwa ameketi pale, nasi tulikuwa na mahindi na maharagwe na—nanyi mnajua jinsi watu maskini wanavyoishi, ndipo—ndipo nikasema, kamwe hatukuwa tumeomba baraka mezani, nami nikasema, "Nyote mtainamisha vichwa vyenu kwa dakika moja?"

153 Nami najua Baba aliniangalia, naye Mama akaniangalia kitofauti. Nikasema, "Mungu, sijui jinsi ya kuomba, lakini *kwa njia moja ama nyingine*, ninakuamini Wewe. Ninaamini ya kwamba Wewe uliniponya, nimetiwa mafuta, nami ninalichukua Neno Lako."

154 Sasa, Mama alikuwa ameniwekea uji wa shayiri na maji ya plamu kavu, na hivyo tu ndivyo nilivyokuwa navyo, nilikuwa nikila hivyo na biskuti za ngano nzima kwa yapata mwaka mzima. Ndipo Mama akasema, "Wewe huninii . . . Utakula nini?"

Nikasema, "Maharagwe na ugali, nipe kipande cha hicho kitunguu."

155 Na, mbona, alikuwa amewazia nilikuwa nimerukwa na akili. Akamwita daktari, daktari akasema, "Kitamwua! Mara hicho kikiingia tumboni mwake," kasema, "kitamwua. Kita—kitampa shida kubwa ya kusaga chakula, atakufa."

Nikasema, "Daktari alisema hivyo, bali nimesikia, naamini, nimepokea, nami nitatenda kulingana na yale ninayoamini." Haleluya! Kweli.

156 Nililisikia, nikatambua *hili* kuwa ni Neno la Mungu, Biblia hii, inatoka katika Biblia, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule. Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Hivyo ndivyo alivyosema. Nilitambua ilikuwa ni Neno la Mungu, ilikuwa ni Mungu akinena nami, kwa hiyo nikaingia kazini. Loo, jamani, kilichotukia! Hakika. Hivyo ndivyo Eliya alivyofanya, hivyo ndivyo Musa alivyofanya, hivyo ndivyo Nuhu alivyofanya.

157 Yohana Mbatizaji, baada ya kutambuliwa kama nabii miongoni mwa watu . . . Loo, mwajua, walidhani Yohana alikuwa ni nabii mzuri, pia, mpaka alipomtambua Yesu na kusema Yeye. . . kwamba huyo Mtoto haramu, ilivyoaminiwa miongoni mwa watu, ya kwamba Jamaa huyo alikuwa ndiye Masihi.

158 Mbona, Yesu alitoka huko nje na kuanza kuwakemea hao makuhani na kadhalika, na, mbona, akasema, "Mbona, Yohana, itakubidi kughairi hayo." Kasema, "Vema, mtu huyo anairarua tu jamii yetu yote hapa. Mbona, yeye anasema ubatizo wa Roho unakuja, na mambo hayo yote namna hiyo, dhabihu itaondolewa, mambo hayo yote ya namna hiyo."

159 Naye Yohana akajibu hivi: "Yeye aliyeniambia huko nyikani, 'Nenda ukabatize kwa maji,' alisema, 'Yule ambaye utamwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.'" Amina. Akasema, "Hayo ndiyo yote ninayofanya. Nilisikia Sauti hiyo nyikani, nikatambua ilikuwa ni Mungu, nami nikaenda nikabatiza. Nilipomwona Roho huyo akishuka, na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto; ninatekeleza tu yale Mungu aliyosema yafanywe." Amina. Naam, aliona, akasikia, akatambua, ndipo akaingia kazini.

160 Hilo ndilo kanisa linahitaji. Tunalisikia, tunalitambua, bali tunaogopa kulitekeleza.

161 Hiyo ndiyo shida ya wagonjwa. Jana usiku hapa, vema, Roho Mtakatifu alikuwa akibatiza mahali hapa tena, nikasema, "Wekeaneni mikono. Ninyi. . . Waaminio wangapi?" Kila mtu wakainua mikono yao. "Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi." Basi mnapaswa kuingia kazini baada ya hapo. Mungu asifiwe, toka tu moja kwa moja, useme, "Hili ndilo." Ingia kazini, hivyo tu.

162 Unasema, "Vema, i—ilinibidi kumeza vidonge *kadhaa*."

163 Loo, vema, ulifanya hivyo, bali si sasa, unaona, ingia kazini juu yake. Amini kwa moyo wako wote, endelea tu kusonga mbele, hakuna mahali pa kusimamia.

164 Yohana alisema, “Ninafanya tu yale Bwana aliyoniambia. Nadhani nilisikia, nikatambua kuwa ni Mungu, nilizaliwa kwa uzazi wa kipekee, nimeishi katika nyika hili tangu nilipokuwa na umri wa miaka tisa. Yeye aliniambia niende nikabatize kwa maji, Kisha akasema, ‘Yule utakayemwona Roho akishuka juu Yake.’

165 “Sijawahi kumwona juu ya yeyote wenu makuhani, sijawahi kuona chochote kama hicho. Kamwe sikusikia Sauti yoyote ikinena kutoka Mbinguni juu yenu nyote ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa Naye, msikieni Yeye,’ si—sijapata kusikia chochote kama hicho juu yenu. Na huyo Ndiye aliyesema hilo, na hiyo ndiyo sababu nilimtambua Yeye akisema Yeye ni Mwana wa Mungu. Ninatekeleza tu yale niliyosikia na nimetambua kuwa Mungu.” Amina.

166 Yesu Mwenyewe, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Nafanya lile tu ambalo Baba ananionyesha.” Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno, isipokuwa Baba amwonyeshe. Baba anatenda kazi, nami natenda kazi hata sasa.” Kwa maneno mengine, Yeye alimsikia Baba akizungumza, alijua ilikuwa ni Baba, Naye akaenda na kutenda tu yale hasa Baba aliyomwambia afanye. Mnaona, unasikia, unatambua, kisha unatenda.

167 Hiyo ndiyo sababu Yeye alienda huku na huku, alikuwa na haja ya kupitia Samaria, Naye akamwona mwanamke huyo pale. Alipitiaje Samaria wakati alipokuwa akienda zake Yeriko? Mnaona, vema, Yeye alipitia Samaria. Kwa nini? Baba alisema, “Kwea uende Samaria. Keti chini pale, ungoje.” Hivyo tu ndivyo alivyojua kufanya, kuketi pale na kungoja.

Huyu hapa mwanamke akaja, Baba akasema, “Huyo ndiye ninayetaka kuzungumza naye, sasa ongea naye.”

Akaanza kuongea naye, na hatimaye akapata shida yake ilikuwa ni nini, akasema, “Nenda, kamwite mumeo.”

Akasema, “Sina yeyote.”

168 Kasema, “Hiyo ni kweli, unao watano. Na yule unayeishi naye sasa, siye wako.” Mnaona, Yeye alisikia, Yeye alijua ilikuwa ni Baba, Naye alikuwa akitenda yale hasa Mungu aliyomwambia afanye. Amina. Hmm! Laiti tungefanya hivyo!

169 Watu mia moja na ishirini walipanda chumba cha juu wakati mmoja, chini ya mateso. Ninaweza kuwazia nikiwasikia watu hao wakija, wakisema, “Mnajua nini? Kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha liko kule juu siku kumi. Wana mpango gani wa chakula?”

Wanafunga.

“Simwoni mvulana wa duka la vyakula akipanda juu kule.”

Loo, la, walikuwa wakifunga, walikuwa wakingojea.

170 Kisha kasema, "Unajua nini? Wako huko juu. Kwa nini? Mbona, wao—wao ni...wamefunga milango kabisa, jamaa asingeweza kuingia mle. Panda maskini vipandio hivi vidogo vya hekalu hapa juu, ni mtu mmoja tu kwa wakati anaweza kwenda kwenye chumba hicho, nasi tukifika kule juu, mbona, huwezi kuingia. Kwa hiyo ni kitu gani...? Afadhali tu waachwe wakae huko juu, nadhani, wafe kwa njaa wakitaka."

171 Kwa nini? Nia ya kimwili. Hata hivyo walikuwa wa kidini, wote walikuwa huko juu kwenye Pentekoste nao walikuwa wa kidini sana, lile kundi la Esau.

172 Lakini, mnaona, kundi la Yakobo lilikuwa kule juu likingojea, kwa sababu walikuwa wamemsikia Mungu akisema, "Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mtakapovikwa uwezo utokao Juu. Akiisha kuwajilia juu yenu huyu Roho Mtakatifu, ndipo mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na pande za mwisho za ulimwengu." Ati nini? Ngojeni kwanza, mwende Yerusalemu, mkangoje huko mpaka ahadi hii itakapokuja.

"Bwana, Wewe ulituita. Hilo si ni zuri vya kutosha?"

"Naam, hilo ni sawa."

"Ulitupa nguvu za kutoa pepo. Hiyo ni kweli?"

173 "Naam, hilo ni sawa, bali ninawatakeni mwende kule mkangojee." Walimsikia Mungu akisema jambo hilo, walitambua ya kwamba Yeye hakuwa mtu haramu, Yeye alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu, naye alijua hiyo ilikuwa hivyo, kwa hiyo wakapanda kwenda Yerusalemu, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Walienda kule na kungojea. Walitambua kuwa ni Mungu, mara wakaingia kazini.

174 Mnajua matokeo yake yalivyokuwa. Waliyumbayumba kama walevi, wakanena kwa lugha, wao, loo, kundi baya sana ulilowahi kusikia maishani mwako, mpaka watu wakasema, "Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya." La... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

175 ...ilikuwa ni Paulo huko nje baharini, tukifunga sasa, Paulo, huko nje baharini, akizitii amri za Mungu. Mungu alikuwa akimtaka aabiri mahali fulani.

176 Wakaachilia ufukoni, lakini Mungu alipomwambia—alipomwambia awaambie, naye akawaambia wasifanye hivyo, lakini nahodha, wao...mnajua yeye alikuwa ni msomi, alijua zaidi kuhusu bahari kuliko Mungu alivyojua, asingeweza kumwamini nabii wa Mungu. Kwa hiyo akaifungua tu meli na kuanza kusafiri, na ilikuwa siku kumi na nne mchana na usiku, hapakuwapo na mwezi wala nyota. Maskini meli hiyo ilikuwa imejaa maji. Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Wakatupa kila kitu baharini, karibu tu hivyo, kupakua shehena. Na ilikuwa, matumaini yote yalikuwa yamekwisha.

177 Ninawazia Paulo alikuwa kule chini akitembea huku na huko kwenye manchani mahali fulani, ama juu kwenye kiambaza cha meli akisema, “Vema, Bwana, nitakuja kwako juu ya bahari, nadhani.” Akitembea tu huku na huku, akiwa na wakati mzuri usiku huo, akishangilia, akikokota minyororo hiyo nyuma yake.

178 Ndipo ghafla kesho yake asubuhi, huyu hapa anakuja mbio juu ya sitaha, maskini mikono hiyo midogo imefungwa minyororo, miguu yake ikijikokota namna *hiyo* ikiwa na minyororo nyuma yake, akiitikisa mikono namna *hiyo*, kama mtu aliyepagawa, na kusema, “Kuwa na ushujaa mwingi. Bwana asifiwe! Haleluya!”

“Una shida gani kijana?” Maskini Myahudi huyo mwenye pua iliyopinda huko juu akitikisa tu mikono yake, na kupiga makelele. “Kuna nini Paulo?”

179 “Kuwa na ushujaa mwingi. Endelea ukale chakula. Hujala kwa muda mrefu sana, umekuwa ukifunga kwa muda mrefu sana sasa, kula chakula. Kuwa na ushujaa mwingi, hakuna kitakachopotea.”

“Mbona una hakika hivi Paulo? Umepatwa na nini? Umerukwa na akili? Labda ulifunga kwa muda mrefu sana mpaka ukaingiwa na kiwewe.”

180 “La, la. La. Jana usiku Malaika wa Mungu, ambaye mimi ni mtumishi Wake, alisimama karibu nami na kusema, ‘Paulo, usiogope.’” Haleluya! “Akasema, ‘Hakutakuwa na yeyote atakayopoteza maisha.’ Nami ninamwamini Mungu, itakuwa tu kama Yeye alivyoniambia.”

181 Ati nini? Alisikia, akatambua kuwa ni Mungu, naye akaingia kazini, kabla ya jambo lolote kutukia. Mwezi ulikuwa mbali sana kama ulivyowahi kuwa, jua lilikuwa jeusi tu kama lilivyowahi kuwa, nyota zilikuwa bado haziangazi, meli ilikuwa tayari tu kushuka chini kama ilivyowahi kuwa, ibilisi alikuwa ameketi juu ya kila wimbi akiwa na wimbo wa furaha kinywani mwake na kuangaza meno yake, huku akisema, “Nitampata kwa linalofuata. Nitampata kwa linalofuata.” Lakini Malaika alimshindia pale. Loo, jamani!

182 Paulo alisikia, akatambua, naye akaingia kazini, kasema, “Haleluya! Ni kama tu tumeketi moja kwa moja ukingoni, sasa hivi.”

“Kwa nini?”

183 “Mungu alisema hivyo. Jambo ndilo hilo. Yote yamekwisha, Mungu alisema hivyo. Niko njiani.” Kwa hiyo, hivyo ndivyo tu ilivyokuwa. Hivyo ndivyo ilivyo daima, kusikia, kutenda, na kuamini.

184 Loo, wakati huu mkuu tuliomo sasa, sasa, nitasema mambo machache makali katika dakika moja, nami ninawatakeni

msikilize, ile siku kuu tunayoishi, nguvu hizi zote zinaushika ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu kuna watu wengi sana wenye wasiwasi, mbona kila kitu, ho—hospitali za wendawazimu zinajaa. Naam, kuna mshiko miongoni mwa watu, hawaelewi ni kitu gani, ni nguvu hizi kubwa zinazofikia kilele. Angalieni hapa, kila kitu kimefika kileleni, kila kitu kiko kwenye mwisho.

185 Angalieni hapa, hebu tuchukue kwa mfano, siasa, siasa katika taifa letu. Ndugu, kama jambo fulani likitukia kwenye huu unaofuata, litahitaji tu kama wimbi moja zaidi, na ni hayo tu. Um-hum. Hivyo tu. Nia ya kimwili, loo, jamani, jinsi wanavyoweza kufanya hivyo! Kila kitu kinajitokeza sawa kabisa kulingana na Maandiko.

186 Siasa zimeoza kila upande. Sheria za serikali, ziangalieni, ziangalieni sheria zetu za miji, zinunue kwa dola kumi. Naam, inategemea unamjua nani, zinunue tu. Mingi sana ya miji yetu iko hivyo nchini, ninajua hilo ni kweli.

187 Nguvu zingine, angalieni nguvu za elimu, angalieni sayansi. Sayansi imeshuka mpaka wamevunja atomi, na molekuli, na kadhalika, mnaona, mpaka wakafikia mahali ambapo uhusiano wa kitaifa umefikia kilele chake. Sasa hakuna kitu. . .

188 Sasa, kati ya mataifa, kuna vurugu, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema ingekuwa, "dhiki kati ya mataifa." Kila taifa dogo linaogopa. Urusi ingesukumia bomu hilo hapa sasa hivi kama hawakuogopa nasi tungewasukumia moja pia. Hiyo ni kweli. Sasa hawajui la kufanya, wako kwenye mwisho wa safari.

189 Sayansi iko mwisho wa safari, loo, uadilifu uko mwisho wa safari, umama na uwanawake uko mwisho wa safari, kanisa liko mwisho wa safari. Kanisa la kimwili linaelekea moja kwa moja kwenye muungano wa makanisa. Hiyo ni kweli kabisa.

190 Nalo Kanisa la kiroho liko mwisho wa safari. Linaelekea kwenye Kilele Chake, kule Kuja kwa Bwana Yesu. Lote linaelekea juu, hiyo ni kweli, linaelekea kwenye Kuja kwa Bwana. Bwana Yesu, Uongozi wa Kanisa unakuja. Yeye atafanya nini? Atawafufua watakatifu wote na kuwapa mwili uliotukuka. Haleluya! Nina furaha kujua ya kwamba linapanda juu. Linapanda juu katika mambo mawili makuu, likija kwenye wakati wa mwisho: alama ya mnyama, na Muhuri wa Mungu.

191 Nao Muhuri wa Mungu, mhudumu yeyote anajua, ya kwamba Muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli kabisa. Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu." Amina. Loo, najua mnafikiri ninatenda kiajabu, labda na—najisikia vizuri. Mnaona? Loo, jamani, kuelekea mwisho!

192 Sasa kumbukeni, alama ya mnyama ni nini? Alama ya mnyama ni Esau wa kimwili kuikataa hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Hivi Esau hakulia kwa uchungu, akijaribu kurudisha

haki ile ya mzaliwa wa kwanza tena, bali hapakuwapo na mahali pa toba? Unapomkataa Roho Mtakatifu, unajitia muhuri nje ya rehema ya Mungu. Amina.

193 Sasa, mnasema, "Sasa, Ndugu Branham, wewe—wewe—wewe. . .Kama ungetwambia magonjwa yetu, na kadhalika, ungekuwa nabii, lakini sasa wewe ni . . . "

194 Vema, mimi—mimi ningali ni mtu yule yule. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ningali nina yale Maandiko yaliyosema, hiyo ni kweli kabisa. Amina. Ingali ni kweli.

195 Na inaelekea kwenye alama ya mnyama. Nao watu wanasema, "Loo, kutakuwako na alama," ta—tayari imetiwa alama. Mkatae tu Roho Mtakatifu, nawe umetiwa alama.

196 Mpokee Roho Mtakatifu nawe umetiwa alama. Amina. Hiyo ni kweli. Upokee mara moja uone kitakachotukia. Upokee mara moja. Hiyo ndiyo alama ya Mungu, nawe umetiwa muhuri hata kikomo chako cha Milele.

197 Kama vile gari huko nje barabarani, mkaguzi anakuja. Sasa, baadhi yenu hamkumpokea Roho Mtakatifu jana usiku, mlioingia mle, chunguzeni usiku wa leo, Mkaguzi, Roho Mtakatifu yuko hapa, kwa namna fulani anakukagua.

198 Nilikuwa nikifanya kazi kwenye Shirika la Reli la Pennsylvania. Tungepakia gari, labda na makopo, na kadhalika, ndipo mkaguzi akaja, angetikisa kila kitu, aone kama kulikuwa na ulegevu wowote. Hivyo ndivyo Mungu anavyolitendea Kanisa Lake, analitikisa, aone shida Yake ni nini, aone kama kuna ulegevu wowote ndani yako, kabla Yeye hajamwaga Roho Wake ndani yako.

199 Na kama kanisa kidogo linatetemeka, Yeye hatamwaga Roho Wake ndani yake. Kama ungali unaupenda ulimwengu, na unataka kufanya mambo ya ulimwengu, kamwe hutampokea Roho Mtakatifu juu ya hayo. Huenda ukapata kuchanganyikiwa, huenda ukapata mdomo wa kugugumiza, huenda ukapata . . . ama huenda ukanena kwa lugha, lakini bado hilo halimaanishi una Roho Mtakatifu. Unapokuwa na Roho Mtakatifu, umetiwa muhuri na Mungu hata kikomo chako cha Milele. Hiyo ni kweli.

200 Wakati mkaguzi huyo alipokuja na kukitikisa kitu hicho, nalo behewa lilikuwa zuri na imara, alifunga mlango, na kuweka muhuri wa Pennsylvania pale, ole wake mtu huyo atakayevunja muhuri huo, mpaka behewa hilo litakapofika kikomo chake.

201 Basi Mungu anapoona ya kwamba umejitolea kabisa Kwake, Naye anakujaza na Roho Mtakatifu, umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu mpaka kikomo chako. Hiyo ni kweli. "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu." Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo hasa, kwa hiyo msiogope, endeleeni tu kusonga mbele. Mpokeeni Roho Mtakatifu, yote yanaishia katika hilo.

202 Jinsi watu walio waaminifu, watoto wa kweli wa Mungu, kile wanachopaswa kuishia siku hizi, kile ulicho nacho mbele yako! Laiti ungalitambua! Kesho usiku ama usiku mwingine au wakati fulani, ninataka kusimulia ono langu, na, kuona kile kilicho mbele yetu; kila kitu kiko mbele. Ni jinsi gani tunavyopaswa kuishi kwa uaminifu kwa ajili yake!

203 Unawezaje wewe, ambaye wakati mmoja ulilipumua Jina la Yesu Kristo, kurudi nje ulimwenguni, na kuipa kisogo Damu hiyo iliyokutakasa? Unawezaje kufanya hivyo? Nimeshawishika kwanza kabisa hukuwa nayo. Hiyo ni kweli. Kila mtu aliyewahi kuonja wema wa Bwana, mbona, mambo ya ulimwengu yanakufa kama usiku wa manane. Hiyo ni kweli. Ingia ndani na umpokee Roho Mtakatifu. Usiigize kanisa, usifanye kama jirani yako, ingia ndani na useme, "Bwana, nataka unijaze na Roho Mtakatifu halisi."

204 Kwa nini uchukue kibadala, kwa kupeana mkono na mhubiri, na kunyunyiziwa mara chache, ama kitu kama hicho? Kwa nini uchukue kibadala cha theolojia ya kanuni fulani ya imani ya kujibunia, wakati mbingu zimejaa nguvu za Kipentekoste, amina, ile Pentekoste halisi ya kweli?

205 Mwaminio ana kitu cha kuishia. Tunapaswa kuishi hivyo, tukipokea kila siku kwa ajili ya kila kitu tunachoweza kupata kutoka kwa Mungu, ukiuacha ulimwengu nyuma, ukiteketeza meli zako kila siku, ukiiteketeza njia nyuma yako, endelea kusonga mbele, ukufikia, ukivuta, ukitafuta, ukiona njaa, ukimwonea Mungu kiu. Kuwa mlokole kabisa kulihusu, endelea tu.

206 *Mlokole* ni mtu mwenye shauku kupita kiasi. Mimi ni—mimi ni. . .mlokole kwelikweli. Nina shauku kupita kiasi juu ya Bwana wangu. Alipataje kuniokoa? Yeye alipataje kunipa Roho Mtakatifu? Kwa nini aliniruhusu kuhubiri? Aliniachaje niwapende watu, na watu wanipende? Loo, nina furaha sana juu Yake, ninaendelea tu kufikia kwa yote yaliyo ndani yangu, nikinyosha ngozi yangu kujaribu kumfikia, nikienda tu na kila kitu nilicho nacho. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya.

207 Inanikumbusha hadithi niliyosikia siku moja. Kundi la wasanii wa Marekani lilishuka kwenda Rumi kusomea sanaa. Niliona katika, ninaamini gazeti la usiku wa leo, ambapo kulikuwa na wasanii fulani wakija katika moja ya miji hii, hapa karibuni sana, kufungua jumba la sanaa. Ninapenda sanaa, Mungu yuko katika sanaa, aina ifaayo ya sanaa; Mungu yuko katika muziki, aina ifaayo ya muziki; Mungu yuko katika kucheza dansi, namna ifaayo ya kucheza dansi; Mungu yuko katika kupaza sauti, namna ifaayo ya kupaza sauti. Dhambi ni upotovu, ni kuchukua kitu kilicho sahihi na kukipotosha.

208 Sasa, kama vile kanisa fulani lilivyokuwa, mtu fulani alinipigia simu, hapa si muda mrefu uliopita, kanisa kubwa, na

ilikuwa kwenye televisheni, jamaa fulani aliniita, kasema, “Njoo hapa, Mhubiri, shuka uje hapa kwa dakika moja. Nataka uone kipindi cha televisheni.”

209 Basi kulikuwako na moja ya madhehebu yetu makuu, kanisani walikuwa na baadhi ya mambo yamefunikwa, jamani, hili halikuwa ni kanisa Katoliki, hili lilikuwa ni kanisa la Kiprotestanti, lilifunika hayo mambo, nalo lilikuwa likifanya mazoezi ya roki. Nao walisema kwamba “Kwa muda mrefu kanisa limeacha na kupuuza sanaa nzuri ya roki.”

210 Kama hiyo si roho iliyopotoshwa, sijui ni nini. Roki ni ya ibilisi. Sijali ni nyimbo ngapi za kidini watu wanaweza kuimba, roki, na bugi-bugi, na upuuzi kama huo unatoka kwenye misitu ya Afrika, hiyo ni kweli kabisa, ni ibilisi.

211 Hiyo ndiyo sababu ninasema jambo hili, hiyo rangi na vipodozi, laiti mngalijua tu mahali hizo zinatoka, ni tabia ya kikafiri. Waangalieni, nendeni huko Afrika mkawaangalie hao wanawake, jinsi walivyotengeneza matope haya na kujipaka rangi, mamia ya miaka kabla bibi yako hajavitumia. Hakika. Mnaona ni kitu gani? Ni cha ibilisi. Hakina shughuli katika makanisa ya Kipentekoste, hakina shughuli katika makundi hayo.

212 Nawaambia, tunahitaji kuoshwa vizuri na Roho Mtakatifu, kote kote kutoka mimbarani, hata kwa bawabu, hiyo ni kweli kabisa, kuoshwa na Roho Mtakatifu, kuwatakasa watu wetu.

213 Wanaume, Wapentekoste, wakisema, “Kamwe siwezi kujizuia kuvuta sigara.” Mtu aliyeoa wake wawili, na kuwa shemasi kanisani: Mfukuzeni, bila shaka, hilo ndilo jambo la kufanya. Huna budi kufanya mambo. . .Biblia ilisema ya kwamba shemasi anapaswa kuwa mume wa mke mmoja. Hiyo ni kweli kabisa. Baadhi yao wana wawili au watatu, katika milki za Kipentekoste. Ndugu, hatuwezi kuwa na uamsho, mpaka tutakapokisafisha kitu hiki. Unawezaje kujenga juu ya msingi usio sahihi?

214 Kama nilivyowaambia jana usiku, Meksiko, huko chini, walijenga mji huo mzuri, lakini walikuwa na hakika sana wangeufanya wa kuvutia sana kwa nje, sasa mji unarudi nyuma, majengo yao makubwa, mazuri yanayumbayumba. Kwa nini? Hawakuufikia msingi. La hasha.

215 Nilimsikia mhudumu fulani hivi majuzi, akimleta mtoto mdogo kwenye simu, ama, maikrofoni, wanne ama watano wa hao, na kusimama pale baada ya yeye kusema hakuna kitu kama baadhi ya fundisho kuu la Biblia. Akamleta huyo mtoto mdogo pale, kisha akachukua chupa ya chumvi, na kuwatupia matone matatu ya maji kichwani mwao, na kusema, “Ninakubatiza, katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Ndipo akampitisha mtoto huyo mdogo kuwa mfuasi wa kanisa, hana umri wa miezi sita bado. Mbona, maskini jamaa huyo

mdogo hana nafasi, kwanza kabisa alianza kwenye msingi mbaya.

216 Hilo hata haliko katika Biblia, hiyo ni desturi ya kikafiri, hata haiko katika Maandiko. Ndugu, kamwe hatutaanza mpaka tutakapoingia kwenye msingi na kuanza vizuri, kujenga kwa Roho Mtakatifu juu ya Neno la Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Hakuna mtu katika Biblia aliyewahi kunyunyiziwa, hakuna kitu kama hicho. Neno la Kiyunani *batiza* linamaanisha, “kufunikwa, kuzikwa, kufichwa.” Kweli kabisa.

217 Sasa, lakini tunafanya nini? Tunapata lundo la kanuni za imani na kadhalika, tunaaza kuziishia, na upuuzi kama huo, “Daktari *nanii* alisema hivyo.”

218 Ninataka kujua yale Biblia isemayo, ninataka kulisikia na kulitambua kuwa ni Mungu kwa Neno Lake, kisha anijalie kuliweka katika matendo.

219 Wasanii hawa, kundi la wasanii, walienda Rumi kusomea sanaa. Wote wangetoka nje usiku, karibu wote, na kuingia katika ulevi mkubwa, wavulana kwa wasichana, na kulala pamoja kama tu baadhi ya Wamarekani wa kisasa wafanyavyo, wanalala nje.

220 Nilienda mahali fulani, hapa katika jimbo lili hili, ambapo walikuwa na mkutano, na sijawahi kuona aibu hivyo maishani mwangu mwote. Kulikuwa na jamaa mkubwa mno ameketi pale amevaa kofia kubwa, wote wamepambwa maua namna hii, na wamevaa majoho ya kila namna, na kadhalika, nao wavulana na wasichana wadogo wa umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba, wakilala pamoja katika chumba cha hoteli. Kesho yake asubuhi, wote wakishuka, wakiinama, na, “Baba *Nanii*.”

221 Loo, jamani! Kuwazia tu, kupotosha akili za maskini watoto hao kwa upuuzi kama huo, wakati Mungu aliwainua kuwa wana na binti za Mungu, ili wawe safi na watakatifu, waliotakaswa kwa nguvu za Mungu, waliooshwa katika Damu ya Mwanakondoo.

222 Ninajua hilo huwafanya watu wanichukie wakati mwingine, bali mtanipenda nitakapokutana nanyi huko ng’ambo. Nitawaambia kweli, ni msingi. Kama ni . . . Haijalishi inagharimu nini, hiyo . . . utakuwa mwaminifu, na kusema kweli. Utambue kuwa ni Mungu. “Iweni watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu,” Yeye alisema, acheni kuishi katika dhambi.

223 Watu hawa wangetoka kwenda kunywa pombe, na kufanya yasiyofaa. Lakini waliona kijana mmoja, kijana huyo, hakutenda namna hiyo. Aliishi safi, usiku alikuja nyumbani na kwenda kulala, aliishi kama muungwana anavyopaswa kuishi. Ndipo siku moja maskini mlinzi akasema, “Napenda kufanya matembezi pamoja nawe, mwanangu.”

Akasema, "Vema." Wakaanza kupanda kilima, wakitembea pamoja kuelekea machweo ya jua.

Naye akasema, "Kijana, ulikuja pamoja na kundi hilo la Wamarekani, sivyo?"

Naye akasema, "Naam, bwana, nilikuja nao."

Akasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani."

Akasema, "Vema."

224 Akasema, "Mbona hutoki nje, na kunywa pombe, na kupiga makelele, kulala nje na hao wasichana, na kadhalika, usiku kucha, na kuja kesho yake asubuhi, jinsi wafanyavyo?"

Akasimama, akamkumbatia huyo mzee, akasema, "Unaona jinsi jua lile linavyotua huko magharibi?"

Akasema, "Naam, bwana, ninaona."

225 Akasema, "Ng'ambo ya hayo machweo ya jua, kuna jimbo fulani, katika majimbo ya New England," kisha kasema, "katika jimbo hilo fulani kuna mji fulani, na katika mji huo fulani, kuna nyumba fulani, na katika nyumba hiyo fulani, kuna msichana, naye msichana huyo, niliweka nadhiri kabla sijaja hapa, kuwa mwaminifu kwake, ya kwamba tutakaponinii . . . Nitakaporudi, tutafunga ndoa. Aliniwekea nadhiri, ahadi. Kwa hiyo, bwana, usikivu wangu wote unavutiwa, tukinena kuhusu wanawake, na msichana huyo mahali hapo." Naye akasema, "Ninaishi leo, kesho ipate kuja." Ni ushuhuda wa jinsi gani!

226 Kile Mkristo anaweza kusema:

227 "Kwa nini huvuti sigara? Kwa nini usijifurahishe kidogo? Kwa nini usifanye *hivi* kama hao wengine wanavyofanya?"

228 Loo, unaweza kusema, "Ng'ambo ya nyota fulani, kuna Mji fulani, na katika Mji huo fulani kuna Mtu fulani. Haleluya! Loo, ninamwishia, kwa kuwa Yeye alikufa kwa ajili yangu, na siku moja Yeye yuaja. Nami ninaishi kwa ajili ya Maisha hayo yajayo."

229 Loo, ndugu, niamini, nakwambia kweli, nakwambia yaliyo kweli. Mungu anajua ya kwamba ninakwambia kweli. Niamini tu kwa moyo wako wote. Labda huwezi kuelewa hili kuhusu Kuja kwa Bwana, na kanisa la kimwili, na kadhalika.

230 Na baadhi yenu, moja kwa moja kutoka kwenye jimbo hili, waliniandikia barua na kusema, "Upako unapokuwa juu yako, unaweza kuzitambua roho," kasema, "basi, bila shaka, sisi, basi tunaamini wewe ni nabii." Sasa, kamwe sikusema mimi ni nabii, mlisema hivyo. Mnaona? Lakini mnasema, lakini basi ninyi mnasema, "Lakini katika mafundisho yako, Ndugu Branham, kuhusu ulokole huo wote kuhusu kumpokea Roho Mtakatifu, na upuuzi huu wote, na kuishi, hatuwezi kuamini hilo. Na upuuzi huu mwingine wote ati wewe uliteuliwa Milele, kabla ya ulimwengu, na . . . "

231 Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema mlikuwa, kamwe sikuwa na chochote cha kusema juu yake, Biblia ilisema hivyo, ninasema tu yale Biblia iliyosema, naam, bwana. “Naye huyo mnyama huwadanganya wote walio juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Hiyo ni kweli.

232 Hiyo ndiyo sababu watu siku hizi, wakati wewe hujaitwa, unawezaje kuja? Hiyo ni kweli. Sijui ni nani aliyeitwa, na ni nani hajaitwa, ninatupa tu wavu, na huenda nikapata kamba, na nyoka, na buibui wa majini, na chochote kile, lakini jambo pekee ninaloweza kufanya ni kuvuta wavu. Mungu Ndiye anayehukumu, hivyo tu.

233 Nitawaambia, Roho wa Mungu yupo hapa. Na ninii... Kama Roho wa Mungu anaweza kuniambia siri ya moyo wako, Roho wa Mungu anaweza kutambua Neno Lake, na kurudi moja kwa moja, na kulihubiri Neno. Sijawahi kuhubiri kitu kingine chochote bado, ila kile kilichokuwa katika Biblia hii, nilidumu moja kwa moja Nayo. Ninaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu.

234 “Ulisema ulikuwa Mbaptisti.”

235 Mimi ni Mbaptisti aliyempokea Roho Mtakatifu. Nilipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninaamini katika Kuja kwa pili kwa Kristo. Ninaamini kila Neno lililoandikwa katika Biblia hiyo na kulihubiri jinsi tu lilivyoandikwa. Sibadilishi jambo moja, wala kulifanya lolote kuwa la kiroho, ninasema tu limeandikwa, hivyo ndivyo ninavyoliamini. Ninalisikia, ninalitambua kuwa ni Mungu, na kuliweka katika matendo. Amina.

236 Roho Mtakatifu ni halisi tu leo kama alivyowahi kuwa. Haitubidi kuwa na imani yoyote ya bandia, ya kujifanya, Roho Mtakatifu halisi yupo hapa. Yesu halisi, Yeye hajafa, Yeye yu hai, hajafa. Aliwaambia wanafunzi, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Ninaamini hilo.

237 Ninaamini ya kwamba Yeye alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao.” Unaamini hilo? Hivyo ndivyo alivyosema, ninaamini hilo. Ninaamini Yeye yupo hapa sasa hivi, sivyo? Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaamini hilo?

238 Kuna mwanamke, wakati mmoja, alijipenyeza na kugusa upindo wa vazi Lake, akageuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Na alipofanya hivyo, ingawa wote waliotazama huku na huku hawakujua la kusema, Yeye alimwona huyo mwanamke na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akaponywa, kasema kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Ninaamini Yesu yuyo huyo ni Kuhani Mkuu usiku wa leo, Yeye yule, Yeye hajashindwa kabisa.

239 Tutakuwa na ibada ya uponyaji moja ya siku hizi usiku, kuwaleta watu huku. Nina huduma mpya niliyopewa. Hiyo ilikuwa huduma yangu ya kale.

240 Aisee, la, hakuna kadi zozote za maombi, sivyo? Hakuna mtu aliye na kadi ya maombi, maana hatuninii, hatujasambaza kadi za maombi. Vema. Kama unaamini ujumbe huu unatoka kwa Roho Mtakatifu. . .Ni wagonjwa wangapi walio hapa ndani? Inueni mikono yenu, kwamba unajua ya kwamba sikujui. Vema. Wewe kuwa na imani na uamini, amini kwa moyo wako wote.

241 Tutaona kama Roho Mtakatifu yeye yule anayehubiri haya mahubiri ni Roho Mtakatifu yeye yule anayejua siri za moyo; tutaona kama Neno huja, Neno la Mungu humjia Nabii au la; na mimi si Nabii, Yeye ndiye, Yeye Ndiye. Wewe amini, kuwa na imani. Bwana Mungu wa Mbinguni na atujalie kwa ajili ya utukufu Wake.

242 Mtaamini hili ni Neno la Mungu ambalo nimehubiri kama Yeye atalifanya? Endeleeni tu kuomba, iweni na kicho kabisa kwa dakika moja, tulieni tu kwa dakika moja. Mtazameni Roho Mtakatifu akitenda kazi juu ya mtu fulani. Endelea tu kuomba, ukisema, "Bwana Mungu, mimi ni mgonjwa, nina haja. Kweli ni—ni—nina haja, Bwana. Si—sina budi kukupata, nisipokupata Wewe, nita—nita—nitaangamia."

243 Mtu huyu aliyeketi hapa, uliinua mkono wako dakika chache zilizopita, bwana? Unainua mkono wako? Unaamini Mungu anakujua? Hatufahamiani, hiyo ni kweli? Sikujui, lakini Mungu anakujua. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Kama nikikwambia shida yako, unaliamini? Itabidi iwe ni kweli kama ndivyo. Unaamini kama Mungu ataniambia hivyo utakubali uponyaji wako? Utaukubali?

244 Unafikiri vidonda vitakwisha? Unafikiri vitapona? Vema. Una vidonda vinavyotokwa na damu. Hiyo ni kweli. Umekuwa mahali pengi sana kwa ajili yake. Ulienda kwa Mayo Brothers, ninakuona ukienda kwa Mayo Brothers. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Nao walikukataa, bali Mungu hakukatai. Unalisikia? Unalitambua? Je, utaliweka katika matendo? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, nenda nyumbani ukawe mzima.

245 Unamwamini Mungu? Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule anayehubiri Neno anafanya uaguzi wake, akilifanya Neno halisi. Akikwambia kufanya nini? Hiyo ni kweli.

246 Kuna mgonjwa mwingine wa vidonda amekaa pale pale, mtu asiyevaa shati, masharubu meusi, ama masharubu, huko nje, hana shati, ukosi uliofunguliwa, ninamaanisha, hapa juu, hana tai ya shingoni kwenye shati lake. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Hatufahamiani, bali una vidonda. Hiyo ni kweli. Nawe unataka kuponywa, sivyo? Wewe hutoki kwenye mji huu, la, unatoka Cleveland. Hiyo ni kweli.

247 Hebu nikwambie jambo lingine: Una leso mbili mfukoni mwako ambazo unataka kunipata, ili niziombee hizo kwa ajili ya wapendwa wawili nyumbani. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hiyo*. Zichukue na uwawekee, watapata afya, pia, BWANA ASEMA HIVI.

248 Mnaamini? Ni Roho wa aina gani anayehubiri? Roho wa namna ile ile anayepambanua.

249 Hapa, yule pale mama mzee ameketi, ameketi moja kwa moja huko nyuma, anamwombea mkwewe aliyejeruhiwa katika ajali ya motokaa; ameketi moja kwa moja kutoka kwenye nguzo hiyo, hapo. Unaamini, dada, kwa moyo wako wote kwamba aponywe? Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuupokea.

250 Huyo mama mnene aliyeketi nyuma yake hapo, ana shinikizo kuu la damu, uliyeketi moja kwa moja nyuma hapa karibu na hii nguzo, kama unaamini kwa moyo wako wote, unaamini ya kwamba kuvuja kwako kutakuacha? Vema, basi unaweza kuupokea. Amina.

Weka mkono wako juu yake. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki, dada. Amina.

Mnampenda?

251 Huko nyuma kabisa nyuma ya jengo, mtu fulani huko nyuma, unamwombea binti ya—yako. Nilitaja ajali muda mfupi uliopita, alikuwa katika ajali, pia, aliumia uti wake wa mgongo. Hiyo ni kweli. Una dada mkwe ambaye ana shida na shingo yake, kichwa pia. Unaamini ya kwamba Mungu atawaponya? Bw. Golden, je, uta—utamtambua Mungu, kuwa ni sauti Yake inayosema nawe? Vema, bwana. Simama kwa miguu yako, basi. Vema. Nenda nyumbani ukawakute wakiwa wazima, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

252 Yesu yeye yule, yeye yule jana, leo, na hata milele! Hivi huwezi kuloweshwa na hilo ndani yako, kwamba ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu? Unaweza kusikia? Je, unaweza kutambua? Basi, liweke jambo hilo katika matendo.

253 Kila mgonjwa aliye humu ndani, Mungu tayari amekuponya wakati alipomtuma Yesu afe kwa ajili yako. Unaamini hilo? Basi simama kwa miguu yako na umkubali Yeye kama Mponyaji wako, na kama Mwokozi wako. Inueni mikono yenu, ingieni katika matendo, tokeni kwenye viti vya magurudumu, chochote kile. Katika Jina la Bwana Yesu, inueni mikono yenu, na kumsifu, na kuamini kwa moyo wako wote.

254 Bwana Yesu, tunawaleta watu hawa Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Nguvu Zako na zitoshe, Bwana, kutujalia hili, na jalia kila nguvu za ibilisi ziachiliwe katika jengo hili usiku wa leo, na jalia watu waponywe.

255 Ninakutoa, Shetani! Ninakuja dhidi yako kwa kesi kwamba wewe ni mdanganyifu. Naja katika Jina la Yesu Kristo

kama mtumishi Wake, ninawaombea watu hawa, huku Roho Mtakatifu akiwatia mafuta, wanasikia, wanatambua ni Mungu, wataliweka katika matendo. Toka, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, waache watu hawa!

256 Na mponywe, kila mmoja wenu. Amina.

257 Ninaigeuza ibada . . .?. . .

60-0607 Kusikia, Kupokea, Na Kutenda
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org